# Nipashe

Jumanne Agosti 13, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581767

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




**VAN DIJK: BADO SIJAPATA OFA YA MKATABA MPYA**

UKURASA 21

UKURASA WA 3

**Watupa** sarafu mtoni wakiamini kutatuliwa shida zinazowakabili

UKURASA WA 5

**Panya** wa SUA kutambua mtu aliyefukiwa na kifusi, nyara katika kontena



UKURASA WA 3

**Polisi** wataja chanzo kifo cha msanii Mandojo

# Vigogo wote wa CHADEMA selo



Joseph Mbilinyi



John Pambalu



Tundu Lissu



Freeman Mbowe

• **Wadau** walaani ukiukwaji R4 za Rais Samia; ACT wazuiwa, Polisi yadai haijazuia mikutano...

*Endelea Uk. 2 & 18*

UKURASA WA 4

## WAGONJWA 102 MNH WAPANDIKIZWA FIGO

## Mkandarasi ang'oa milango kituo cha afya akishinikiza alipwe deni milioni 200/-

UKURASA 18

## DK. BITEKO AZINDUA TAWI JIPYA LA KCB BANK GEITA

**Na Mwandishi Wetu,**
GEITA

KCB Bank imepanua huduma zake kwa kufungua tawi jipya huko Geita, ikithibitisha dhamira yake ya kujumuisha kifedha wananchi wa Tanzania.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nshati, Mhe. Dkt. Doto Biteko, ameipongeza KCB Bank kwa kuendelea kuwekeza nchini, hatua ambayo imeleta athari chanya kwa biashara na maisha ya wananchi wa Geita....

ENDELEA UKURASA 2



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akizindua tawi la KCB Bank mkoani Geita. Pamoja naye ni Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba, Mkurugenzi wa Biashara za Kanda wa KCB Group na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya KCB Tanzania, Cosmas Kimario na Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigela. Tawi hilo jipya litasaidia kuchochea shughuli za kiuchumi mkoani humo pamoja na kurahisisha upatikanaji huduma za kifedha kwa wananchi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

**MICHEZO** **SIMBA SASA YALETA STRAIKA MCAMEROON** UK.24 **MAONI,** UK.6



Mbunge wa Viti Maalumu anayewakilisha kundi la watu wenye ulemavu, Stella Ikupa, akizungumza katika kongamano la kitaifa la watu wenye ulemavu, wadau na madiwani Dar es Salaam jana, lililolenga kusikiliza changamoto za watu wenye ulemavu. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Vigogo wote CHADEMA selo

**Na Waandishi Wetu,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limeimarisha ulinzi katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya kwa lengo la kudhibiti wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) waliokuwa wamepanga kufanya maandamano huku likikamata vigogo wote wa chama hicho.

Wanachama wa chama hicho walipanga kufanya maandamano ya amani katika maeneo mbalimbali ya jiji hilo kisha kufanya kongamano kwenye Uwanja wa Ruanda Nzove jijini ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Vijana Duniani.

Hata hivyo, kutokana na kauli zinazodaiwa kuwa na utata za baadhi ya viongozi wa chama hicho, Jeshi la Polisi nchini kupitia Kamishna wa Operesheni na Mafunzo, Kamishna wa Polisi Awadh Haji lilipiga marufuku shughuli za chama hicho.

Kamishna Haji alisema jeshi hilo liliamua kupiga marufuku mikutano na mikusanyiko ya ndani na nje baada ya intelijensia kubaini kuwa kauli za viongozi wa CHADEMA zinaashiria kuwa kunaweza kukatokea uvunjifu wa amani.

Pamoja na katazo hilo la Jeshi la Polisi, pia Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, ilielekeza viongozi wa chama hicho kusitisha kongamano hilo kwa madai kuwa kauli zilizotolewa na baadhi ya viongozi zilikuwa zinakiuka Sheria ya Vyama vya Siasa.

Jana maafande wa Jeshi la Polisi walionekana wakiwa wameimarisha ulinzi katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya ikiwamo katika Uwanja wa Ruanda Nzovwe ambako CHADEMA walipanga kufanyia kongamano lao.

Katika uwanja huo hapakuwa na wanachama wa CHADEMA wala viongozi isipokuwa askari polisi waliokuwa wamejihami na silaha za moto pamoja na mabomu ya machozi huku wakizuia waandishi wa habari kuwapiga picha.

Uwanja huo pia kulikuwa na magari matatu ya polisi ambayo moja ni la maji ya kuwasha na mawili ni ya kawaida, likiwamo la OCD Njombe yakiwa yameegeshwa.

Hatua chache kutoka kwenye uwanja huo pembezoni mwa Barabara Kuu ya Tanzania na Nzambia (TANZAM) karibu na Kituo cha Daladala cha Mama John, lilionekana gari lingine la polisi lililokuwa na maandishi yanayosomeka OCD Mbozi likiwa na askari.

Vilevile, kwenye Ofisi za CHADEMA Kanda ya Nyasa zilizopo Kadege, jijini, walionekana askari wakiwa wametanda kila kona wakilinda usalama huku ikiwa haijulikani kama kwenye ofisi hizo kulikuwa na watu.

Mbali na maeneo hayo, pia yalionekana magari ya polisi yakiwa yamejaa askari waliorandaranda mitaani na vituo vya daladala, hasa katika Jiji la Mbeya na katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi.

Hata juzi usiku ziliibuka taarifa kwenye mitandao mbalimbali ya kijamii kuwa baadhi ya viongozi wa juu wa CHADEMA walikuwa wanashikiliwa na polisi akiwamo Makamu Mwenyekiti, Tundu Lissu, Katibu Mkuu, John Mnyika na Katibu Mwenezi wa Baraza la Vijana (BAVICHA), Twaha Mwaipaya.

Jana mchana, ziliibuliwa taarifa kuwa Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe ambaye alitarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye kongamano hilo, alikamatwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA) wakati akitua kwa ajili ya kwenda jijini Mbeya.

Nipashe lilimpigia simu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP) Benjamin Kuzaga kwa lengo la kupata taarifa kuhusu mwenendo wa tukio hilo, lakini simu yake haikupokewa.

Jana ilithibitishwa na chama hicho kuwa viongozi tisa wa CHADEMA na waandishi wa habari wawili, walikuwa wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Mbeya wakati wakiwa katika maandalizi ya kufanya kongamano la vijana wa chama hicho, ambalo lilipigwa marufuku na Msajili wa Vyama vya Siasa na Polisi.

Viongozi hao ni Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Mbowe, Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa Bara, Tundu Lissu, Katibu Mkuu wa CHADEMA Taifa, John Mnyika, Mwenyekiti wa BAVICHA, John Pambalu na Mwenyekiti wa Kanda ya Nyasa, Joseph Mbilinyi, maarufu kama Sugu.

Wengine waliokamatwa ni Wakili Deogratias

Mahinyila, viongozi wa BAVICHA, Twaha Mwaipaya, Moza Ally, Deusdedith Soka na waandishi wa habari wa Jambo Tv ambao ni Ramadhan Khamis na Fadhil Kirundwa.

Taarifa za kukamatwa kwa viongozi hao zilisambaa kwenye mitandao ya kijamii kwa makada wa chama hicho, Martin Masese, Mwenyekiti wa Kanda ya Kaskazini wa CHADEMA, Godbless Lema, ambaye aliandika: "Mwenyekiti Freeman Mbowe pamoja na Mwenyekiti wa Vijana John Pambalu wamekamatwa katika uwanja wa ndege wa Songwe Mbeya."

Kabla ya kukamatwa, jana Mbowe aliandika kwenye ukurasa wake wa X kuwa: "Tunalaani vikali Jeshi la Polisi kukamata viongozi wetu wakuu wa chama ikiwamo viongozi wa BAVICHA. Chama kinafuatilia kwa makini yanayoendelea na kitaendelea kuuhabarisha umma kila linalojiri hatua kwa hatua."

Chama cha ACT-Wazalendo pia kililaani kukamatwa viongozi hao na kutaka waachiwe kwa kuwa waliofanya hivyo, wanakinzana na falsafa za 4R za Rais Samia Suluhu Hassan, ambazo ni Ustahimilivu, Maridhiano, Mabadiliko na Kujenga Taifa Upya.

Walisema vitendo vinavyofanywa na polisi vinaonesha hatua chache za kuimarisha uhuru wa kujumuika, kukusanyika na kujieleza viko shakani.

Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Olengurumwa pia hayuko nyuma katika suala hilo; jana alinukuu Ibara ya 18 na 20(1) ya Katiba ya nchi inayotoa haki na uhuru wa watu kujumuika, kufanya mikutano, maadhimisho na kueleza mawazo yao.

"Haki hizi hazipo kwenye Katiba peke yake, bali zipo kwenye mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda ambayo Tanzania imeridhia," alieleza katika tamko lake.

Alisema ukamatwaji huo unafifisha uhalisia wa maridhiano, ustahimilivu na mabadiliko ambayo Rais Samia amekuwa anasisitiza tangu alipoingia madarakani.

"Tunatoa wito kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini kuwaachilia huru watu wote waliokamatwa bila masharti ili kuadhimisha Siku ya Vijana Duniani kama ambao vyama vingine vimeshaadhimisha na hatukuona wakikamatwa," alisema.

Juzi, Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi, Kamishna wa Polisi Awadh Haji, alisema jeshi hilo liliamua kupiga marufuku mkutano huo kutokana na matamko yanayotolewa na viongozi wa chama hicho kuashiria uvunjifu wa amani.

Wakili wa CHADEMA, Philip Mwakilima, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema viongozi na wanachama wanaoshikiliwa kwenye vituo vya polisi tofauti ni 117.

"Hadi sasa sijui wamehifadhiwa wapi, awali tuliambiwa wako Mbalizi na tulivyofuatilia hawakuwapo. Tangu tulipoanza kufuatilia hatujaelezwa sababu za kuwashikilia. Baadhi ya viongozi wanaoshikiliwa wanatumia dawa, lakini hawajapewa nafasi kuzitumia, pia wengine wanatakiwa kwenda kliniki," alidai.

Hadi jana saa 12:15 jioni, Kamishna alikuwa hajazungumza na waandishi wa habari kama alivyoahidi, na waandishi waliendelea kusubiri katika Ofisi za Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya.

**Imeandaliwa na Nebart Msokwa na Neema Hussein.**

## DK. BITEKO AZINDUA TAWI JIPYA LA KCB BANK GEITA

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

KCB Bank imepanua huduma zake kwa kufungua tawi jipya huko Geita, ikithibitisha dhamira yake ya kujumuisha kifedha wananchi wa Tanzania.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nshati, Mhe. Dkt. Doto Biteko, ameipongeza KCB Bank kwa kuendelea kuwekeza nchini, hatua ambayo imeleta athari chanya kwa biashara na maisha ya wananchi wa Geita.

"Ninaipongeza Benki ya KCB kwa hatua hii muhimu. Tawi hili jipya litaleta fursa kwa wakazi wa Geita kupata huduma za kibenki ambazo zitachochea shughuli za kiuchumi na biashara katika eneo hili," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Biashara za Kanda wa KCB Group na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya KCB Tanzania, Cosmas Kimario, alieleza kuwa tawi jipya la Geita linaendana na mkakati wa KCB wa kueneza huduma zake, na kutoa suluhisho za gharama nafuu na zenye teknolojia ya kisasa ili kuendeleza uchumi jumuishi kifedha.

"Kwa kufungua tawi hili huko Geita, Benki ya KCB inalenga kuleta ukuaji wa kifedha na ubora wa huduma kwa jamii ya eneo hili. Tawi hili litawapa wakazi wa Geita fursa ya kupata mikopo, akiba, na huduma nyingine za kifedha zilizoundwa kuboresha ubora wa maisha yao na kuchochea biashara na fursa za uwekezaji."

Tawi la KCB Geita linafanya jumla ya matawi ya Benki ya KCB Tanzania kufikia 17 nchi nzima, yakiwamo matawi matatu -Arusha, manane Dar es Salaam moja Morogoro, Kilimanjaro, Kahama na Zanzibar, pamoja na mawakala zaidi ya 500 nchi nzima.

Mnamo Oktoba 2022, KCB Bank ilifikia thamani ya mali ya TZS trilioni 1.5 na kuifanya kuingia katika kundi la benki kubwa nchini.

Benki ya KCB imekuwa kiongozi katika kuendeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) kupitia miradi mbalimbali ya kijamii, ambayo imeleta athari kubwa kwa maisha ya wengi, hasa vijana na wanawake.

**Mnamo Oktoba 2022, KCB Bank ilifikia thamani ya mali ya TZS trilioni 1.5 na kuifanya kuingia katika kundi la benki kubwa nchini.**

HABARI KITAIFA



Mwonekano wa Daraja la J.P Magufuli (Kigongo - Busisi) kilometa 3.2 linalojengwa kuunganisha Barabara Kuu ya Usagara - Sengerema - Geita kupita Ziwa Victoria na ujenzi wa barabara unganishi ya kilometa 1.66, utekelezaji wake ukiendelea na sasa kufikia asilimia 90. **PICHA: UJENZI**

## Polisi waeleza chanzo kifo cha msanii Mandojo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma, limetaja sababu za kifo cha msanii wa nyimbo za Bongo Fleva, Joseph Francis maarufu Mandojo, kuwa ni kukutwa kwenye kibanda cha mlinzi ambaye aliita mwizi na watu kujitokeza na kumshambulia.

Mandojo anadaiwa kuuawa kwa kupigwa na watu wasiojulikana kwa kutuhumiwa kuwa ni mwizi katika uzio wa Kanisa Katoliki eneo la Nzuguni B, jijini Dodoma.

Aidha, taarifa kutoka eneo hilo zinadai kuwa msanii huyo alikwenda kanisani hapo kwa ajili ya kusali.

Akizungumza na Nipashe, Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Dodoma, Kamishna Msaidizi Mwandamizi, Anania Amo, alisema Mandojo alikutwa na mlinzi wa eneo hilo majira ya saa 10:00 alfajiri ndani ya kibanda chake.

Alisema baada ya mlinzi kuona hivyo, alipiga kelele kisha watu waliokuwapo eneo hilo na wengine wanaodhaniwa kuwa ni waamini wa kanisa hilo waliokuwa kanisani, walimshambulia kwa kumpiga hadi kufariki dunia.

"Mandojo alituhumiwa mwizi, mlinzi alipopiga kelele kwa muda ule watu walijitokeza na kuanza kumshambulia kwa kipigo kilichosababisha umauti kumkuta, baada ya kubainika amefariki dunia mwili wake ulipelekwa katika Hospitali ya Rufani Dodoma," alisema Kaimu Kamanda Amo.

Hata hivyo, alisema ni kosa kisheria watu kujichukukia sheria mkononi.

"Ni vyema wangemkamata na kumpeleka katika kituo cha polisi kilichoko eneo la karibu, sio kujichukulia hatua mkononi kama walivyofanya," alisema kamanda huyo.

Mtu wa karibu na Mandojo, aliyezungumza na mwandishi wa habari hii kwa sharti la kutotajwa jina, alisema msanii huyo alikwenda kanisani humo kwa ajili ya kusali na kuomba toba kutokana na ugomvi uliokuwa baina yake na mkewe.

Alisema lengo la Mandojo halikutimia na matokeo yake alikutwa na mauti, na kuzima ndoto na mipango yake.

# Watupa fedha mtoni kutatuliwa shida zao

**Na Neema Hussein,** KATAVI

WASWAHILI wanasema, "Ukistaajabu ya Mussa utayaona ya firauni". Baadhi ya abiria katika treni inayopita Kijiji cha Katambike, Kata ya Ugala, wilayani Nsimbo, mkoani Katavi wanadaiwa kurusha sarafu katika Mto Ugala kwa imani kuwa watatatuliwa matatizo yao.

Inadaiwa kuwa watu hao hutumwa kufanya hivyo na waganga wa kienyeji kwa kuwa "ndio sadaka kwa miungu iliyoko katika mto". Hutupa sarafu za Sh. 50, 100, 200 na 500.

Nipashe imetembelea eneo hilo na kuzungumza na wasafiri na viongozi mbalimbali ambao wamelitaja ni jambo ambalo limekuwapo kwa muda mrefu kwa wenye imani hizo.

Eneo hilo ambalo ni maarufu kwa jina la "Tutani", treni inapofika hapo, abiria wenye imani hiyo hurusha sarafu kupitia madirisha ya mabehewa ya treni kama njia ya kutimiza matakwa ya waganga wao.

"Ni kweli hapa pana desturi ya watu kutupa fedha tutani; iwe treni inayotoka Mpanda kwenda Tabora wanatupa au inayotoka Tabora kwenda Mpanda wanatupa pia.

"Hii desturi haijaanza leo wala jana, ni ya enzi na enzi, wanafanya hivyo kwa sababu watu wengi wanapokwenda kuchukua dawa kwa mganga wa kienyeji wanaulizwa 'unasafiri kwa njia gani?', akijibu treni anaambiwa 'hii dawa ili ikafanye kazi kule unakokwenda lazima ukifika kwenye Mto Ugala utoe sadaka ya fedha', fedha yoyote ile,"alisema Michael Jakabwe, mkazi wa Katambike.

"Iwe Sh. 50, mia (Sh. 100), mia tano na sana fedha zinazotupwa pale zilizo nyingi sana ambazo tunazishuhudia ni 50, 100, 200 na 500, zinatupwa sana.

"Unakuta mtu amebeba dawa ya kilimo, maana kwenye kilimo watu wanatumia dawa ili wapate mazao. Mfano, amebeba dawa ya kilimo na ili dawa ikubali kwenye mazao yake, lazima aitolee kafara ya fedha na hili jambo halijaanza leo.

"Wengine wanabeba dawa za biashara, mganga anakwambia 'ukifika Mto Ugala sharti utupe fedha na anatoka amejiandaa kabisa na ile fedha ameiandaa kaiweka labda mfuko wa nyuma na zile fedha mara nyingi wanaambiwa zisichanganywe na fedha nyingine.

"Wasipotoa kafara pale, wanaaminishwa kuna mzimu mkubwa unakaa kwenye mto ambao unaitwa "Silongwe", hivyo wasipotoa sadaka ya fedha ule mzimu utazuia dawa zao zisifanye kazi maana ule mzimu utachukia 'kwanini wapitishe vitu vyao bila kutoa kafara'.

"Nikwambie tu ukweli, asikudanganye mtu zile fedha zina madhara kwa sababu wanaozitoa wanakuwa wamenuia, anayenuiza ni yule aliyeagizwa na mganga wake pale kuna watu wanakwenda kuokota zile fedha wanapata madhara.

"Mfano, juzi tu hapa hata mwezi mmoja haujapita, kuna mtoto aliona fedha baada ya maji kupungua, akaenda kuichukua, yule mtoto alitumbukia kwenye maji na kufariki dunia," alidai.

Hata hivyo, serikali haimini katika uchawi. Kuamini uchawi pia ni kosa la jinai kwa mujibu wa sheria za nchi.

Salumu Katema, mkazi mwingine wa eneo hilo alisema: "Hiyo ni imani kwa kuwa wengi wanapotoka Mwanza na baadhi ya mikoa mingine ya Kanda ya Ziwa wanakuwa wamebeba dawa katika mabegi, wanaambiwa 'mkifika pale Ugala msipotupa hela, zile dawa mlizobeba zinafia palepale, zinakosa nguvu'.

"Kwa hiyo, mtu akifika pale anachukua fedha anarusha kwenye maji au inaangukia kwenye mawe, asubuhi watu wanajipatia ridhiki. "Mara nyingi mimi huwa ninasafiri kutoka Mpanda kwenda Kaliua, tukifika pale Ugala watu wengi huwa tunatupa fedha, hata mimi huwa ninatupa.

"Ni utaratibu ambao tumezoea ila inasemekana pale kuna mizimu kwa hiyo watu wanatupa vile kwa ajili ya matambiko," alisema Milimo Saidi, Mkazi wa Mpanda.

"Unatupa hela yoyote, hata Sh. 10,000 haulazimishwi utupe sarafu tu, ni wewe mwenyewe utakayotaka, hata zaidi ya Sh. 10,000 kwa sababu ukitupa isipokwenda majini, watu wanachukua na wanatumia.

"Sisi tumekuwa tunaokota pale hizo fedha, tunazitumia hatujawahi kudhurika, hata watoto huwa wanakwenda pale wanajua kuna fedha," alisema Kashinde Mayanda, mkazi wa Ugala, akibua hoja inayokinzana na mtangulizi wake aliyedai kuna madhara kuchukua fedha zinazotupwa mtoni huko.

Mzee wa Kimila, Ibrahim Chatama alisema hicho kijiji kimeitwa Katambike kutokana na matambiko yanayofanywa hujko; kwamba ukifika pale wenyeji wanakwambia 'nenda ukatambike'. "Zamani elimu ilikuwa ndogo, watu walikuwa wanafuata mila zaidi kuliko elimu, mila zingine zilikuwa zinafuatwa, zilikuwa halisia, zingine zilikuwa potofu, zilikuwa haziwezi kusaidia wananchi.

"Sehemu ile ya kijiji kilipo, kuna mto ambao ni Ugala, ni mrefu sana. Miaka ya nyuma wakati wanatengeneza reli kutoka Kaliua kuja Mpanda, sehemu ile iliwasumbua sana makandarasi, wakitengeneza tuta, asubuhi hawalikuti hata kama hakuna mvua.

"Ilibidi waende wakawaone wazee kwenye kijiji hicho hicho, wakaambiwa 'hapa si mahala pa mchezo kuna mzimu unaitwa "Silongwe", bila kuuomba reli hii haitapita, sharti uombe kwa kutumia fedha na fedha zilizokuwa zinatumika zamani ni zile nyeupe (sarafu) zenye nembo ya Mwenge upande mmoja na upande mwingine kichwa cha Baba wa Taifa. Baada ya kufanya hivyo, reli ikakamilika.

"Binadamu wengi tuna imani za kimila hususani wale wote wanaokuwa na dawa za kienyeji wanaambiwa 'wewe mkeo si anaumwa sana au mtoto anaumwa, basi chukua hii dawa ila ili uifikishe salama, ukifika pale Ugala sharti uombe ule mzimu ukupitishie salama'," alidai.

Alisema kuwa zamani treni ilikuwa ikipita zile fedha zilizotupwa zilikuwa haziokotwi, lakini hivi sasa imekuwa fursa, kuna vijana wanakuwa pale treni ikipita watu wakirusha fedha, wanaokota na kuzifanyia matumizi yao na hawadhuriki, hakuna madhara yoyote.

Kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, fedha ni tunu ya Taifa na kila mmoja ana wajibu wa kuilinda na kuitunza. Ni kosa la jinai kutupa au kuharibu fedha sarafu au noti.

Kifungu cha 332A cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16, kinaelekeza: "Mtu yeyote, bila mamlaka, kwa kunuwia anaharibu, anachana, anakata au vinginevyo anachanachana noti yoyote ya benki au fedha ambayo inatumika kihalali, atakuwa anatenda kosa ambalo limo kwenye jedwali, na atakuhumiwa kutoa faini ya Sh. 5,000 kwa kila noti iliyoharibiwa au akishindwa adhabu ya kifungo cha mwaka moja."

HABARI KITAIFA

# Wagonjwa 102 wapandikizwa figo Muhimbili

**Na Christina Mwakangale**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) Upanga na Mloganzila imefanya upandikizaji figo kwa wagonjwa 102 tangu kuanza kwa huduma hiyo mwaka 2017.

Naibu Mkurugenzi Mtendaji MNH-Mloganzila, Dk. Julieth Magandi, aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu upandikizaji huo unaifanya Mloganzila kufikisha idadi ya wagonjwa 10 kati ya hao.

"Idadi ya wagonjwa wote waliopandikizwa figo inafikia 102 kwa MNH-Upanga na Mloganzila tangu huduma hizo zilipoanza mwaka 2017. Kunaifanya hospitali hii kuwa ndio pekee iliyopandikiza wagonjwa wengi wa figo nchini," alisema Dk. Magandi.

Alisema kuwa kwa mara nyingine MNH-Mloganzila imefanya huduma ya kibingwa na bobezi ya upasuaji kupandikiza figo kwa wagonjwa wawili huku figo ikivunwa kutoka kwa mchangiaji kwa kutumia njia ya kisasa ya tundu dogo (Hand Assisted Laparascopic Donor Nephrectomy).

Dk. Magandi alisema huduma hiyo imefanywa na wataalamu wa ndani kwa kushirikiana na Mtaalamu Mbobezi wa Upasuaji wa Matundu Madogo kutoka Korea Kusini, Prof. Park Kwan Tae.

"Upandikizaji huu ulifanywa mwishoni mwa mwezi Julai mwaka huu, wale waliopandikizwa figo waliruhusiwa ndani ya wiki moja kutokana na afya zao kuimarika, upandikizaji huu umewezekana kutokana na uwekezaji uliofanywa.

"Umehusisha kusomesha wataalamu, kununua vifaa tiba, dawa na vitendanishi pamoja na kuweka mazingira wezeshi na rafiki ya kutoa huduma hii hospitalini hapa," alisema Dk. Magandi.

Alitoa wito kwa umma kujitokeza kuchangia ndugu zao figo na kwa kufanya hivyo kutawapunguzia gharama za uchujaji damu na muda wanaoutumia kupata huduma za kuchuja damu ambao huchukua takribani saa tatu kwa mgonjwa mmoja.

Bingwa wa Magonjwa ya Figo hospitalini huko, Dk. Immaculate Goima, alisema miongoni mwa sababu za magonjwa sugu ya figo ni unywaji pombe uliokithiri, uvutaji sigara, matumizi holela ya dawa za kutuliza maumivu, presha na unywaji holela wa dawa za kienyeji.



Timu ya Madaktari Bingwa wa Upasuaji wa Mfumo wa Mkojo na Figo kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)-Mloganzila, wakiendelea na upandikizaji figo kwa mgonjwa ambaye figo yake imeshindwa kufanya kazi. **PICHA: MNH-MLOGANZILA**

# Waziri ataka wazazi kuandaa jina la mtoto kabla hajazaliwa

**Na Kulwa Mzee**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Pindi Chana, ameomba wazazi kuandaa majina ya watoto wao kabla ya kuzaliwa ili kwa haraka wasajiliwe na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa baada ya kuzaliwa.

Balozi Dk. Chana alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dodoma wakati wa ziara yake ya kujionea usajili unavyoendelea na kuwapatia vyeti vya kuzaliwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika Hospitali ya St. Gemma, Kituo cha Afya Makole na Zahanati ya Kikuyu, jijini humo.

"Leo nimetoa vyeti vya kuzaliwa kwa baadhi ya kinamama walioijifungua salama na kuruhusiwa kwenda nyumbani. Ninaomba wazazi kujenga utaratibu wa kuandaa jina la mtoto mapema kabla ya kuzaliwa ili asajiliwe baada ya kuzaliwa na kupatiwa cheti kwani ni haki ya kila Mtanzania," alisisitiza.

Waziri Chana alielekeza taasisi za umma na binafsi kupokea vyeti hivyo vinavyojazwa kwa mkono na kutolewa kwa wototo wa umri chini ya miaka mitano wanaosajiliwa katika ofisi za watendaji kata na vituo vya tiba kote nchini kwa kuwa ni vyeti halali na vina hadhi sawa na vyeti vinavyotolewa kwa njia ya kompyuta.

Balozi Dk. Chana pia aliwataka wananchi kuchangamkia huduma hiyo inayotolewa bure nchi nzima, akisema kuwa vyeti hivyo vina mchango mkubwa katika kupata huduma mbalimbali, ikiwamo matibabu kupitia bima ya afya, elimu na baadaye ajira na kuzitaka taasisi mbalimbali za umma na binafsi kupokea vyeti hivyo kwa ajili ya kuwapata wananchi huduma.

"Nipende kupongeza Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) kwa kazi kubwa wanayoifanya ikiwa ni pamoja na kuhakikisha Watanzania wanapata vyeti vyao vya kuzaliwa na hili nimejiridhisha pasi na shaka kazi hii kubwa ikiendelea kwa ufanisi mkubwa," alisema.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Makole, Dk. Flora Mwakalago alisema kuwa tangu kuanzishwa huduma za usajili wa vizazi kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano mwaka 2019, zaidi ya watoto wachanga 550-600 huzaliwa kila mwezi huku kati yao, watoto 200- 250 wakipatiwa vyeti vya kuzaliwa.

"Kwa kipindi cha mwezi Julai 2023 hadi Juni 2024, tayari tumeshasajili na kuwapa vyeti vya kuzaliwa watoto zaidi ya 2,750. Haya ni matokeo mazuri kwa kituo chetu," alisema Dk. Mwakalago.

Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Kikuyu, Dk. Azania Silliah alisema kata ya Kikuyu Kaskazini ina jumla ya wakazi 14,654 (wanawake 9,250).

"Kuanzia mwezi Julai mwaka jana (2023) mpaka kufikia mwezi Juni 2024, tumesajili na kuwapatia vyeti watoto zaidi ya 642 sawa na asilimia 92," alisema Dk. Silliah.

Mmoja wa wazazi waliopatiwa vyeti, Halima Abdallah, mbali ya kushukuru serikali kwa kuboresha na kujenga vituo vya afya, alisema kuwapo huduma hiyo inayotolewa bure nchi nzima kumekuwa mkombozi kwa kuwa kila mtoto anapata cheti cha kuzaliwa mara tu baada ya kuzaliwa na hivyo kuokoa gharama ambazo zingezitumika kukipata kwenye ofisi za RITA.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa RITA, Frank Kanyusi, alisema tangu zoezi hilo la kusajili watoto wote chini ya miaka mitano, watoto wengi wamesajiliwa nchini nzima na mwamko umekuwa mkubwa.


UBALOZI WA MAREKANI, UHOLANZI (EKN), UNICEF, HELIOS TOWER (HTT)
NA
UMOJA HOUSE JOINT MANAGEMENT COMMITTEE
DAR ES SALAAM

**MNADA WA HADHARA:**

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na **Ubalozi wa Marekani, Uholanzi, European Union (Diplomat), UNICEF, HTT na Umoja house** watauza kwa mnada wa hadhara Fanicha, Magari na Generator tarehe 17 August, 2024 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street. **Fanicha na Computer zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi:** Sofa sets, Recliner, Chest drawer, Book case, Meza za ofisi, Viti, Steel file cabinet, Vitanda, Magodoro, Fridge double door Up Right Freezer, Washer, Dryer, Majiko ya Gas/Umeme, Meza za garden, Viti vya garden, Used roofing sheets, Photo copy Mc: Canon, Nashuatec MP6500 na Xerox 7970, Laptops, Computer set, Printer HP Laser Jet, Flat TV, Mashine za GYM, A/c split unit,na vingine vingi.

**Magari na Genereta yataanza kuuzwa kuanzia saa 6:00 mchana:**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Toyota Land Cruiser V8 Station Wagon | 1VDO Diesel Engine | 2009 | Umelipwa |
| 2 | Mitsubishi Pajero Shogun | 4M41 Diesel Engine | 2010 & 2013 | Haujalipwa |
| 1 | Nissan Patrol Station Wagon | TD42 Diesel Engine | 2011 | Umelipwa |
| 2 | Generator KVA 500KVA – 3 Phase | Perkins Diesel Engine | - | Haujalipwa |
| 1 | Generator 150KVA 3 Phase | John Deer Diesel Engine | - | Haujalipwa |
| 1 | Generator 8KVA | Kubota Diesel Engine | - | Haujalipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia tarehe 14 mpaka 16 August 2024, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari au Generator atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 4 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 22 August, 2024 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari au Genereta litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya **VISA na Master cards za CRDB na NBC** yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa lazima kuwa na bid namba itakayopatikana getini na kuvaa barakoa.

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE DAR ES SALAAM**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA**
**CELL NO: 0754 284 926** **E-mail: universalauction@hotmail.com**
**Insta: universalauctioncentre**

## SUA yaja na teknolojia ya panya kutambua binadamu waliofukiwa

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

CHUO Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), mkoani Morogoro kupitia Taasisi yake ya Kutatua Matatizo ya Kibinadamu (APOPO), kimegundua teknolojia ya mpya ya panya buku kuwa na uwezo wa kubaini binadamu waliofukiwa na kifusi kama mbwa wanavyofanya ili kuwaokoa.

Panya hao pia wana uwezo wa kutafuta na kubaini nyara za wanyamapori zilizohifadhiwa katika kontena na kusafirishwa kwa magendo kwenda nchi mbalimbali duniani.

Hatua hiyo inatokana na panya buku hao kupatiwa mafunzo maalumu kupitia mradi huo wa APOPO kwa kushirikiana na wataalamu wa SUA na panya hao kuonesha mafanikio makubwa kwenye kutambua vitu mbalimbali.

Akizungumza na Nipashe wakati wa Maonesho ya Wakulima na Wafugaji ya Kanda ya Mashariki yanayofanyika Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, mjini Morogoro, Mkufunzi Mwandamizi wa Panya kutoka Mradi wa APOPO, Abouswai Msuya, alisema panya hao wana uwezo wa kusaidia binadamu kwenye mambo mbalimbali.

Msuya alisema panya hao wameonesha uwezo wa kutambua binadamu waliofukiwa na kifusi kwa kuingia ndani na kuonesha walipo baada ya kufungwa kifaa maalumu, ikiwamo kamera.

"Hicho kifaa na kamera, panya anavishwa kikiwa na mfumo usiohitaji waya, unakiweka kama vile unavyotumia kompyuta, ni kama mtandao fulani kwa ajili ya mawasiliano baina ya panya na mkufunzi wake, hivyo anavyokwenda ndani ya kifusi kumtafuta na akimbaini tu kuna ishara fulani itamjulisha mkufunzi na hivyo panya huyo atarudi na kupokea zawadi na kisha kwenda kutafuta mtu mwingine," alisema Msuya.

Alisema panya hao ni wa kawaida, lakini wanachukuliwa wakiwa wadogo na kufundishwa mafunzo tofauti, wapo wanaofundishwa kijeshi na wengine wanafundishwa masuala ya afya ikiwamo kubaini vimelea vya ugonjwa wa kifua kikuu (TB) na mabomu yaliyotegwa ardhini.

Kuhusu nyara za serikali, mkufunzi huyo alisema wapo wanyama kama kakakuona ambao wapo katika hatari ya kutoweka, hivyo wamewafundisha panya hao kunusa kontena bandarini ambalo linatumika kusafirisha wanyama hao nje ya nchi.

Alisema panya buku hao wana uwezo wa kubaini na kutambua meno ya tembo, kifaru na magamba ya kakakuona yanayofishwa katika kontena bandarini na viwanja vya ndege. Ufanisi wao kiutendaji ni wa asilimia zaidi ya 80.

Mkurugenzi wa APOPO, Christophe Cox akizungumza wakati wa maadhimisho ya miaka 25 ya taasisi hiyo ambayo inafanya kazi na SUA kupitia mradi wa kufundisha panya buku, alisema wameandaa miradi mitatu, ukiwamo wa kufundisha panya buku kutambua na kutafuta meno ya tembo, kifaru na magamba ya kakakuona.

Alisema ubunifu huo umekuja kutokana na nyara za wanyama hao kusafirishwa kwa magendo kupitia bandari na viwanja vya ndege kwenda nchi mbalimbali duniani. Wanashirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA).

"Katika wiki ya mwisho ya mafunzo ya panya buku, TAWA walificha sampuli ya meno ya tembo, kifaru, magamba ya kakakuona na panya wetu wamepata asilimia 84 ya sampuli hizi na matokeo hayo ni ya kuvutia kwani ilikuwa ni kwa mara ya kwanza na muda huo ulikuwa ni joto jijini Dar es Salaam kwa nyuzi 35," alisema.

Makamu Mkuu wa SUA, Prof. Raphael Chibunda, alisema chuo hicho kimekuwa na uhusiano mzuri na APOPO na ana imani kuwa miradi inayokuja itaisaidia jamii na nchi kwa ujumla.

Alisema kupitia mradi huo wa APOPO wamefanikiwa kuwapata wagonjwa 25,000 kupitia uwezo mkubwa wa panya buku kubaini vimelea vya TB katika sampuli zilizoshindikana kwa maabara za hospitalini.

# Ukaguzi mabasi ya shule wapamba moto Muheza

- Polisi waonya mabasi ya wanafunzi kutumika shughuli za harusi, misiba

**Na Steven William,** MUHEZA

WAMILIKI wa mabasi ya shule wilayani Muheza, mkoani Tanga wametakiwa kuyapeleka magari yao kwa ajili ya ukaguzi na watakaokaidi, watachukuliwa hatua.

Agizo hilo lilitolewa jana na Mkuu wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani wilayani Muheza, ASP Leonard Bandola, wakati wa ukaguzi wa baadhi ya magari ya shule katika Uwanja wa Jitegemee, wilayani hapa, akisisitiza kuwa suala hilo ni la lazima na lipo kwa mujibu wa sheria.

ASP Bandola alisema ukaguzi huo ni wa kawaida kwa mujibu wa sheria na unafanyika miaka yote.

Alisema anatoa wito kwa wamiliki wote wa mabasi yanayobeba wanafunzi lazima wayapeleke polisi kukaguliwa mara kwa mara.

Kamanda Bandola alipiga marufuku mabasi yote ya kubeba wanafunzi kutumika kubeba abiria, shughuli za harusi au misiba.

Vilevile, kiongozi huyo wa polisi aliagiza wamiliki hao wa mabasi ya kubeba wanafunzi kuhakikisha wanayafanyia matenengezo kwa kiwango cha juu ili kusitokee ajali kwa watoto ambao ni taifa la kesho.




Naibu Katibu Mkuu Bara wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Benson Kigaila, akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, kuhusu kukamatwa kwa viongozi na wanachama 443, pia alitoa rai kwa polisi kuwaachia wanachama hao. Kulia ni Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje, John Mrema. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Kituo cha kudhibiti umeme kwenye gridi kujengwa Dom

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, amesema kituo kikubwa cha kudhibiti mfumo wa umeme kwenye Gridi ya Taifa kitakuwa jijini Dodoma badala ya kile kilichoko Ubungo, Dar es Salaam hivi sasa.

Akizungumza baada ya kutembelea kituo cha kudhibiti mfumo huo wa umeme Ubungo, Dk. Biteko alisema kituo hicho cha Ubungo ambacho ndicho kikubwa na kinachotegemewa kwenye Gridi ya Taifa, kitakuwa cha ziada baada ya kumalizika ujenzi wa kituo cha Dodoma.

Alisema mpango wa serikali ni kuwa na vituo vingine vya kudhibiti mfumo wa umeme kwenye kanda mbalimbali, ili kuepusha tatizo la nchi kuingia kwenye giza pale kinapoharibika kituo kikubwa tegemewa cha gridi hiyo.

"Kituo kikubwa cha kudhibiti mfumo wa umeme nchini cha Ubungo ndicho kinachoona umeme wote nchi nzima. Kiu yetu sisi ni kutengeneza vituo vya kudhibiti gridi ya nchi kwenye kanda, ili kama kutatokea tatizo mahali fulani, basi vituo kwenye kanda nyingine viwe na umeme.

"Ndio maana mtaona kwamba tunajenga kituo kikubwa cha Dodoma, hiki cha Ubungo kitakuwa kidogo ambacho kwa Dar es Salaam kitabaki kuwa 'backup', lakini tutajenga pia vituo vya namna hiyo upande wa kaskazini - Arusha, Tanga na Kilimanjaro, Mikoa ya Kusini, Kanda ya Ziwa ili ikitokea shida yoyote mahali popote, basi nchi nzima isiingie katika giza kwa sababu ya kituo kimoja kuharibika," alisema.

Dk. Biteko alisema tayari Shirika la Umeme (TANESCO) limefanya kazi nzuri ya kuandaa stadi, hatua iliyofikia katika kujenga kituo hicho kikubwa cha gridi cha Dodoma ni kutafuta mkandarasi.

"Hizi ni kazi ambazo zinahitaji fedha nyingi sana, muda na umakini, nichukue nafasi hii kushukuru Wizara ya Fedha, Rais Samia Suluhu Hassan kwa msukumo wake mkubwa wa kuimarisha nishati katika nchi yetu, tunataka Watanzania wapate umeme wa uhakika wakati wote," alisema Dk. Biteko.

"Kipindi hiki kuna matatizo madogo yanayotokea kwa sababu ya matengenezo, watuvumilie, tuimarishe, Mungu ametusaidia tuna ziada ya umeme, ndio maana leo kuna baadhi ya mitambo tumeizima kwa sasa kwa sababu umeme tunao wa kutosha, hatuhitaji kuwasha mitambo yote," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni wakati wa kuchangamkia kilimo cha parachichi

**MATUNDA** ya parachichi yametokea kupendwa na soko lake ni kubwa duniani kutokana na faida zinazopatikana kwenye tunda hilo.

Kwa Tanzania tumebahatika kuwa na mikoa ambayo zao hilo linastawi vizuri na utafiti unaonesha kuwa parachichi kutoka nchini kwetu lina ubora kulinganisha na nchi zingine zinazozalisha tunda hilo.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa amewahimiza wananchi wa Mkoa wa Iringa na Watanzania kwa ujumla kuingia kwenye kilimo cha matunda hayo kwa kuwa zao hilo linachochea ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Serikali imefanya juhudi katika kipindi cha miaka mitatu, kutafuta masoko kwa ajili ya maparachichi yanayozalishwa nchini badala ya kutegemea nchi jirani pekee.

Nchi ambazo kuna soko la uhakika ni China na India kutokana na thamani kubwa na ubora wa hali ya juu ya maparachichi yanayozalishwa Tanzania ukilinganisha kutoka nchi nyingine.

Watanzania wametakiwa kuingia kwenye mpango wa kuzalisha miche ya zao hilo ili kuongeza idadi ya uzalishaji wa maparachichi. Hiyo ni kutokana na ubora mkubwa. Na hii ni baada ya kupima udongo nchini kote na kubaini kuwa Tanzania ina maeneo yenye udongo unaofaa kwa kilimo hicho.

Pamoja na kuhimiza kilimo hicho, pia suala la miundombinu ya barabara lazima lizingatiwe ili matunda hayo yatakapofikia msimu wa mavumo yasiozee mashambani kwa kushindwa kusafirishwa kwa sababu ya ubovu wa barabara.

Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) pamoja na Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), wana jukumu kubwa la kuhakikisha miundombinu ya barabara inapitika vizuri.

Tanzania ina baraka ya kupata ardhi nzuri ya mazao na mavuno mengi, lakini tatizo kubwa ni usafirishaji wa mazao kwenda sokoni kutokana na barabara mbovu ambazo wakati wa mvua hali huwa mbaya zaidi. Tatizo hilo husababisha wakulima kupata hasara kutokana na mazao mengi kuozea kwenye maghala au mashambani kwa ugumu wa kusafirisha kupeleka sokoni.

Hivyo, ni muhimu wakati wananchi wanahamasishwa kujihusisha na kilimo hicho, ni vyema iende sambamba na kasi ya utengenezaji wa miundombinu ya kusafirisha mazao hayo.

Pia, wananchi wapewe elimu ya kutokukubali wafanyabiashara wanaokwenda kuwarubuni kwa kununua mazao yakiwa hayajakomaa na kuuza kwa bei ya chini.

Ni habari njema kutoka kwa Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde, kuwa serikali imeshasaini mkataba na kampuni ya Afac Engineering ambayo itajenga kiwanda cha kusindika maparachichi katika eneo la Nyololo ambapo katika awamu ya kwanza, Sh. bilioni 3.4 zitatumika.

"Wana-Mufindi ni watu wanaolima sana, Mbunge wenu amesimamia ahadi ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ya kujenga kiwanda cha kusindika maparachichi. Mkataba ulishasainiwa na kabla ya Ijumaa ijayo, tutamkabidhi eneo mkandarasi ili aanze kazi."

Kujengwa kwa viwanda vya kuchakata matunda ni njia nzuri ya kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa nchini badala ya kuuza ghafi.

Wanunuzi wa bidhaa zetu ghafi kwenda kuzichakata na kuja kuziuza nchini kwetu kwa bei za juu, ni hali ambayo inapunguza pato la nchi.

Aidha, ujenzi wa viwanda vya kuchakata mazao utasaidia kuokoa yale mazao yanayooza yakiwa shambani. Vilevile, kuongeza thamani ya zao husika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Tuntule Swebe

# Tunufaike sasa na 'Swahili' dijitali

**MIAKA** ya 1950 Umoja wa Mataifa (UN), ulianza kukiona Kiswahili kuwa kina nafasi kubwa ya kuwa moja ya lugha bora za Kiafrika duniani na inayoweza kuunganisha watu wengi.

Ni wakati huo ukaanzisha kitengo cha lugha ya Kiswahili cha Redio ya Umoja wa Mataifa na hata sasa Kiswahili ndiyo lugha pekee ya Kiafrika iliyomo katika kurugenzi ya mawasiliano ya kimataifa ndani ya UN.

Mambo yameendelea kuwa mazuri kwa Kiswahili pale Baraza Kuu la Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) lilipopitisha azimio la kukifanya Kiswahili kuwa na siku maalumu duniani.

Ndiyo maana Julai 7 kila mwaka dunia inaadhimisha Siku ya Kiswahili duniani. Kwa Tanzania ni 'Kiswahili Day' na Sabasaba pia.

Pamoja na sikukuu ya wafanyabiashara, taifa linashiriki kwenye majukumu ya kitaifa na kimataifa katika kukienzi na kutambua mchango wa lugha hiyo katika kukuza utamaduni, ushirikiano na kujenga uelewa na ujuzi wa mambo mbalimbali.

Katika kusherehekea Siku ya Kiswahili duniani pekee hakutoshi, hivyo ni wakati wa kujipanga na kuchangamkia fursa za Kiswahili kidijitali ili kunufaika na lugha hiyo inayotumika karibu kila mahali duniani.

Watanzania wana nafasi ya kuwafunza wengine Kiswahili, iwe Afrika, Ulaya, Amerika na Asia hasa China na India.

Ni mwanzo wa kupata ajira kupitia kuandika na kutafsiri mambo mbalimbali kwa Kiswahili na kuongeza matumizi, kusoma na kujifunza lugha hiyo.

Kama taifa ni vyema kuwa na mkakati wa kutumia lugha hii kuendeleza Watanzania. Kuna haja ya kuwaandaa wanafunzi katika ngazi ya sekondari waanze kuweka mkazo maalumu kwenye somo hilo.

Wataalamu hao watafanikisha juhudi za taifa za kuwa na vijana wanaomudu Kiswahili kuanzia kufundisha, kitaifa na kimataifa, kuongea na kukitafsiri kwa lugha mbalimbali kwenye majukwaa ndani na nje ya mipaka.

Ikumbukwe kuwa, iwapo vijana hao wataandaliwa ipasavyo, inawezekana kwenda sehemu mbalimbali za Afrika na mabara mengine kufundisha lugha hiyo na Tanzania ikapokea walimu wa lugha nyingine kama Kifaransa na Kiingereza kutoka mataifa wanayobadilishana.

Mathalani, Rwanda na Burundi inaweza kubadilishana na Tanzania walimu wa Kiswahili na pia ikailetea walimu wa kufundisha Kifaransa na Kiingereza.

Kiswahili, kinatumiwa kwenye majukwaa ya kimataifa mfano UN na Umoja wa Afrika (AU) yote hayo ni fursa za ualimu, kutafsiri au ukalimani.

Kiswahili kidijitali kinaibua fursa mbalimbali za ajira hasa kwa kufundisha somo hilo kwenye vyuo na taasisi za elimu nje ya Tanzania.

Kwa kuwa Kiswahili ni miongoni mwa lugha za kimataifa na Azimio la UNESCO linalenga kutambua kuwa ni kati ya lugha za Kiafrika zinazotumiwa zaidi, Kusini mwa Sahara mwa Afrika iwe chachu ya kukitumia kubadili maisha.

Kama ni lugha ya mawasiliano katika nchi nyingi za Afrika Mashariki, Kati na Kusini, Watanzania wanangoja nini?

Kiswahili ni lugha rasmi ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), hivyo kukifanya kuwa fursa ya kazi Zimbabwe, Malawi na Zambia.

Kadhalika ni lugha rasmi ya Afrika Mashariki (EAC) ni muda wa kuona namna ya kufikisha Kiswahili Somalia, Sudan Kusini na pengine Ethiopia.

Juhudi hizo ni lazima ziendane na kujua Kiingereza kwa ufasaha, pamoja na Kifaransa hata Kiarabu na Kichina ili kazi ya kuwa mwalimu wa Kiswahili iwe nyepesi.

Ukumbuke katika kufundisha Kiswahili ni lazima kwanza kujua lugha ya mawasiliano ya taifa ya unaowafundisha hatua kwa hatua uitumie kuwafundisha Kiswahili.

Ni kama unatafsiri kutoka kwenye lugha yao na kuwafundisha kile unachokusudia .

Kazi za sanaa za Kiswahili nazo zina nafasi ya kuwapa Watanzania ajira kuanzia kuandaa sinema, kutunga nyimbo zenye mseto wa Kiingereza, Kifaransa, Kichina na Kiarabu ambazo zitawavutia wasikilizaji wengi duniani yaani 'kolabo' zikihusisha wasanii wa mataifa mbalimbali.

## Watanzania wafanya maandamano ya hisani Kenya kuombea uchaguzi

**Na Mwandishi Wetu,** MOMBASA

RAIA wa Tanzania ambao ni waumini wa taasisi ya dini ya New Life Prayer Centre and Church ya jijini Mombasa, Kenya, wamefanya maandamano ya hisani katika kanisa hilo kuombea nchi yao amani wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwaka huu na mwakani, mtawalia.

Walifanya maandamano hayo jana katika viunga vya makao makuu ya kanisa hilo jijini Mombasa, wakirejea historia kwamba zipo baadhi ya nchi ambazo zimekuwa zikiingia vitani mara baada ya uchaguzi.

Kingozi wa kanisa hilo, Mch. Ezekiel Odera, alisema amani ni nguzo muhimu kwa anayepigiwa kura, anayepiga kura na wale watakaoongozwa.

Alisema Tanzania inajulikana kwamba ni nguzo ya amani katika Bara la Afrika, sababu ambayo imekuwa ikivutia wengi kupenda nchi hiyo, akiwamo yeye ambaye mara kwa mara amekuwa anaendesha mikutano yake ya huduma za kiroho.

"Kwa mwaka jana nilifanya mikutano minne Tanzania na miwili hapa kwetu Kenya. Na watu wengi wamekuwa wakiniuliza kwanini ninapenda sana Tanzania na mimi ninasema 'mahali alipo Mungu, amani ipo na mwanadamu akijua alipo Mungu ni lazima atamfuata'.

"Ninafurahi pia kuwaona Watanzania wanakuja kwetu tufanye maombi ya kuomba amani, wametupenda, tumewapenda," alisema mchungaji huyo.

Mratibu wa kanisa hilo kwa upande wa Tanzania, Nabii Utukufukwabwana Peter alisema kwa kawaida silaha hutengenezwa wakati wa amani na kutumika wakati vita, hivyo ni muhimu kufanya maombo kipindi hiki ili Tanzania iendelee kuwa na amani wakati na baada ya uchaguzi.

Alisema amani ni moja ya tunu za Taifa la Tanzania, ambayo Rais Samia Suluhu Hassan anafanya juhudi kubwa kuilinda na kuidumisha, hivyo waumini hao wanamuunga mkono kupitia huduma za kiroho.

"Watanzania kutoka takribani mikoa yote tumesafiri kuja huku ili kufanya maombi haya pamoja na kiongozi mkuu wa kanisa letu, ambaye amekuwa karibu na taifa letu wakati wote, iwe shida au raha.

"Tutakumbuka wote kwamba nchi yetu ilipopata majanga ya kuporomoka kwa tope wilayani Hanang, mkoani Manyara, kiongozi wetu mkuu wa kanisa alikuwa Tanzania, akaguswa na ajali hiyo na kuchukua jukumu la kuchangia zaidi ya Sh. milioni 100," alisema.

Kwa niaba ya Watanzania wenzake, Rose Godfrey kutoka Bomang'ombe, mkoani Kilimanjaro, alisema waumini wanaamini kila kitu kinawezekana kupitia maombi ya kanisa hilo kama ambavyo yalimponya yeye saratani ya kizazi.



Mkurugenzi wa Sab Investments, Saida Bwanakheri (kulia), akizungumza na washiriki wa mafunzo maalum ya ufugaji kuku wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo, wilayani Kisarawe, Mkoa wa Pwani jana, yatakayofanyika kwa muda wa mwezi mmoja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbinu kuimarisha kinga homa ya nyani zatolewa

**Na Jenifer Gilla**

WADAU wa afya wameshauri jamii kuendelea kuchukua tahadhari ya ugonjwa wa homa ya nyani kwa kula vyakula vyenye kuongeza kinga ya mwili na kuepuka kugusana.

Ushauri huo umekuja ikiwa ni takribani wiki mbili tangu serikali itahadharishe wananchi kuhusu ugonjwa huo ulioripotiwa katika nchi jirani za Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Ofisa Mawasiliano ya Afya Wakati wa Dharura Wizara ya Afya - Idara ya Kinga, Sehemu ya Elimu ya Afya kwa Umma, Oscar Kapera, alisema mwishoni mwa wiki kuwa licha ya kuwa ugonjwa huo haujaingia nchini, ni muhimu wananchi, hasa wanaoishi mipakani kuchukua tahadhari.

Alisema ugonjwa wa homa ya nyani husababishwa na virusi vinavyojulikana kama 'monkey pox' na huambukizwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu au kutoka kwa mtu mmoja kwenda mwingine kwa kugusana na mtu mwenye dalili za ugonjwa.

Alitaja dalili kuu ya mtu mwenye ugonjwa wa mpox ni kuwa na vipele maeneo mbalimbali ya mwili, ikiwamo uso, mikono, miguu na sehemu za siri.

"Vipele hivi hufanana na vipele vingine ila huweza kutofautishwa kwa kuwa vinaambatana na kuvimba, homa, maumivu ya kichwa, vidonda kooni, maumivu ya viungo vya mwili ikiwamo misuli na mgongo," alisema.

Aliongeza kuwa mtu yoyote anaweza kupata ugonjwa; wale ambao kinga ya mwili ipo chini wapo kwenye hatari zaidi ya kupata ugonjwa huo.

Daktari Bingwa wa Tiba ya Familia kutoka Hospitali ya Agakhan, Willbroad Kyejo, alisema ugonjwa huo unaweza kuzuiliwa na usisambae nchini kama hatua stahiki zitachukuliwa na kila mmoja kutimiza wajibu wa kujikinga.

Alishauri kila mmoja kuzingatia kanuni za afya, elimu ya afya na maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya, huku akitaja mambo ya kuzingatia kuwa ni pamoja kuepuka kugusana na mtu anayeonesha dalili za ugonjwa huo.

Alishauri pia kuepuka kugusa wanyama wa porini, hasa wale wanaoonesha dalili za ugonjwa na kuhakikisha nyama ya porini inapikwa vizuri kabla ya kuliwa.

Alishauri wanaohudumia wagonjwa mwenye dalili za homa ya nyani, kama vile vipele na vidonda, wahakikishe wanavaa vifaa vya kujikinga kama barakoa na glavu.

"Pia epuka kugusa ngozi ya mtu mwenye dalili hizi bila kinga sahihi," alisema na kushauri wale waliopo katika hatari ya kupata ugonjwa huo kupatiwa chanjo.

Alisisitiza pia ni muhimu kunawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji safi na yanayoririka, kutumia vitakasa mikono pamoja na kuepuka kugusa majimaji ya mwili, ikiwamo damu, vipele, mate na manii ya mtu mwenye dalili za ugonjwa huo.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, pamoja na mawaziri wa afya wa nchi za Afrika wanatarajiwa kukutana kwa dharura kabla ya mwisho wa mwezi huu kujadiliana na kupitisha mikakati ya pamoja na kuchukua hatua za haraka kukabiliana na ugonjwa huo.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Maabara inayotumia akili mnemba kuanza

**Na Pilly Kigome,**
DODOMA

MAABARA ya kisasa itakayokuwa na uwezo wa kukuza na kusaidia kuongoza utafiti wa masuala ya afya na kilimo kwa kutumia akili mnemba (AI), inatarajiwa kuanza kutoa huduma katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Maabara itakuza utafiti wa uwezo wa binadamu kwenye uvumbuzi wa utandawazi katika kukuza na kuendeleza teknolojia nchini.

Italenga kuwaleta pamoja wasomi, viwanda na Taasisi za Umma nchini Tanzania ili kuendeleza ubunifu wa AI unaotokana na utafiti ambao unachangia katika sera zinazozingatia ushahidi na kijinsia.

Mtaalamu wa Akili Mnemba, Mhadhiri Salim Diwani kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika chuo hicho.

Alisema maabara hiyo inakuja kuunda suluhu katika maeneo hayo kulingana na mahitaji maalumu eneo la Anglophone katika Afrika na itapatikana chuoni hapo.

Diwani ambaye ni mratibu wa huduma za afya katika Maabara ya Utafiti ya AI4D UDOM, alisema maabara hiyo itawezesha nchi zote za Afrika zinazoongea lugha ya Kiingereza kufanya utafiti wao katika maabara hiyo.

Alisema maabara hiyo ipo moja kwa nchi za Anglophone na nyingine kwa nchi za Afrancophone.

"Kwa nchi za Anglophone, Tanzania imepata bahati ya kuwa na maabara hiyo na itakuwa UDOM. Udhamini wa kujengwa kwa maabara hiyo umepatikana kutoka IDRC-Canada kwa ajili ya matumizi ya tafiti ya akili bandia pekee," alisema na kuongeza:

"Maabara hiyo kwa sasa itakuja na tafiti za kilimo na afya ambapo itaweza kuitangaza Tanzania katika teknolojia ya AI na sisi tumebahatika kujengewa kwa ufadhili kutoka Canada baada ya awali kufanya vizuri katika tafiti za mwanzo," alifafanua.

Maabara hiyo kwa kupitia wataalamu wake bobezi tayari wameshatengeneza zana za afya (AI-HealthCare Tool for Maternal complications and Child Health Risks) kwa ajili ya kuangalia matatizo ya dharura kwa wajawazito na watoto kwa kutumia Akili Mnemba.

"Zana hizo zinatarajiwa kufanyiwa majaribio kwenye hospitali mbalimbali nchini Tanzania. Zikipitia majaribio hayo, hospitali zitakuwa na wajibu ya kuruhusu na kuanza kuzitumia. Hizi zana zitawawezesha wataalamu wa afya kutambua matatizo ya uzazi katika eneo hilo na kuwezesha kumlinda mjamzito na watoto wadogo," alisema.

Alifafanua, kifaa hicho kiko tayari kimeshatengenezwa na wako katika hatua za mwisho za majaribio. Kutumika kwake itategemea sera za nchi upande wa akili mnemba.

"Kifaa hiki kitakachotumia akili mnemba kitakuja kuwasaidia wataalamu wa afya kugundua shida ambazo zinamnyemelea mjamzito au zitakazompata baadaye baada ya kujifungua kwa kutumia kifaa hicho kitawasaidia wataalamu kuchukua tahadhari kabla ya madhara hayo," alisema.

Kwa upande wa kilimo maabara hiyo itakuja na suluhisho ya zana maalumu ambazo zitakuwa gunduzi katika mazao yote ya kilimo kugundua magonjwa yatakayoweza kuathiri mazao shambani kabla hayajafikia mazao hayo ikiwamo vifaa maalumu vya kusaidia shughuli za shambani kama kuvuna na nyinginezo.

Alisema kwa ushirikiano wa Wizara ya Afya, mpango huu unalenga kuunda muundo unaounga mkono ushirikishaji wa teknolojia za AI kuboresha ufanisi na uhusiano wa utoaji wa huduma za afya kuhakikisha suluhu za kiutamaduni na muktadha kwa jamii ya eneo hilo.

Aidha, maabara hiyo itagusa nyanja tofauti kwa kusaidia sekta mbalimbali ikiwamo utafiti wa benki, viwanda biashara kwa kuandaa mifumo ambayo itasaida sekta hizo kutokana na uhitaji uliopo.



Ofisa Elimu (Sekondari) wa Manispaa ya Kinondoni, Mtundi Nyamhanga (mwenye skafu), akipokea maelezo kutoka kwa Mkuu wa Programu wa Shirika la Realising Education for Development (READ) Tanzania, Anthony Edward, alipozindua maktaba ya Shule ya Sekondari ya Magomeni Makuti Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Ujenzi huo umefanywa na shirika hilo kwa kushirikiana na Kampuni ya Deloitte. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jafo aagiza kampuni za madini kukaguliwa

**Na Faustine Feliciane**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Selemani Jafo, ameiagiza Tume ya Ushindani wa Biashara Tanzania (FCC) kufanya ukaguzi kwenye kampuni za madini ili kubaini yaliyoungana bila kufuata sheria.

Akizungumza jana baada ya kutembelea ofisi za Tume hiyo jijini Dar es Salaam ikiwa ni mara ya kwanza tangu alipoteuliwa kuwa waziri wa wizara hiyo, Jafo, alisema zipo kampuni kwenye sekta ya madini na sehemu nyingine ambazo zimeungana kiholela na kuikosesha serikali mapato yake.

"Pamoja na kazi nzuri mnayoifanya FCC, naomba niagize kwako DG (Mkurugenzi Mkuu), mwende mkafanye ukaguzi kwenye makampuni ya madini, yapo yaliyoungana na kuendelea kufanya biashara bila kufuata utaratibu..., nendeni mkafanye ukaguzi na kufanya tathmini ni kiasi gani cha pesa serikali imekoseshwa," alisema Jafo.

Aidha, aliitaka tume hiyo kuendelea kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi ili kuvutia wawekezaji hasa kwenye uwekezaji wa viwanda.

"FCC ikifanya kazi yake na wawekezaji wakazidi kuongezeka, tutakuwa tumesaidia kuzalisha ajira nyingi kwa Watanzania, tuisaidie serikali katika hili," alisema Jafo.

Mwenyekiti wa bodi ya tume hiyo, Dk. Agrey Mlimuka, alimhakikishia Waziri Jafo kutekeleza maagizo yote aliyoyatoa.

"Tutafanya kama ulivyotuagiza, nikuhakikishie waziri, tuna wafanyakazi wanaojituma na kufanya kazi usiku na mchana," alisema Mlimuka.

Aidha, Mkurugenzi Mkuu, William Erio, alisema kazi kubwa ya Tume hiyo ni kumlinda mlaji na kuweka mazingira wezeshi ya kuwekeza.

Alisema wataendelea kuisaidia serikali kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na kuruhusu ushindani unaotakiwa kwenye biashara.

## Shule yakabidhiwa madawati 150 Mafia

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bima ya Relience imetoa madawati 150 yenye thamani ya Sh. milioni 80 kwa Shule ya Msingi Kiengeani, wilayani Mafia mkoani Pwani, ikiwa ni jitihada za kuunga mkono serikali.

Madawati hayo yalikabidhiwa jijini Dar es Salaam kwa Ofisa Elimu wa Awali na Msingi ya Wilaya ya Mafia Mwalimu, Mathew Mkali kutoka kwa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Bima ya Reliance, Ravir Shankar.

Kampuni hiyo iliamua kutoa msaada huo baada ya kuona mdau mmoja wa maendeleo kutoka wilayani Mafia akisambaza video fupi ikionyesha wanafunzi wa Shule ya Msingi Kiegeani wakikaa chini wakati wa masomo yao.

Aidha, Mtendaji Mkuu wa Kampuni hiyo, Ravir Shankar akiongea wakati wa kukabidhi madawati hayo alisema kuwa ni fursa pekee kwa kampuni yao kuendeleza jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan ya kuweka mazingira bora ya elimu nchini.

Alisema kuwa kuweka mazingira bora ya elimu sio kuwa na majengo au walimu bali hata kuwapa msaada wa madawati wanafunzi ili waje kuwa viongozi na wazalendo wa nchi yao.

Alisema kampuni itaendelea kutekeleza majukumu kwa jamii hususani katika sekta mtambuka, ikiwamo kuchangia Kituo cha Afya cha Eye Charitable Centre kilicho chini ya Jumuiya ya Khoja Shia Ithnaashari kilichopo Temeke wakati wa kuadhimisha miaka mitatu ya kituo hicho tangu kuanzishwa kwake kiasi cha milioni 50.

Ofisa Elimu wa Awali na Msingi, Mwalimu Mathew Mkali, Alisema alikuwa akiwasiliana na wadau mbalimbali katika kukwamua changamoto hiyo ya wanafunzi wa shule hiyo kukaa chini.

Alisema aliwasiliana na mdau mkubwa wa maendeleo katika Wilaya ya Mafia, Hajiankeki Alibhai kuhusu changamoto zinazowakabili wanafunzi hao ndipo mdau huyo alipowasiliana na kampuni hiyo ili kupata msaada huo.

Mdau wa maendeleo katika wilaya hiyo, Hajiankeki alisema sio mara ya kwanza kutafuta wadau na kwenda wilani Mafia kwa kuwa alishafanya Kliniki ya Macho wilayani humo, kujenga visima 12 katika soko la samaki na ujenzi wa kisima cha maji ya kunywa katika Gereza la Wilaya ya Mafia.



## Bil.38/- kujenga miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji

**Na Allan Isack,** KARATU

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 38 kwa ajili ya kujenga miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji katika Halmashauri ya Karatu mkoani Arusha ili kuinua zao la kitunguu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Karatu, Juma Hokororo, alitoa taarifa hiyo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Sisi tumewekeza sana katika kilimo cha zao la kitunguu kwa kuwa halmashauri yetu inaongoza kulima na kuzalisha kitunguu bora," alisema.

Hokororo alisema takribani asilimia 40 ya mapato ya halmashauri hiyo yanatokana na kilimo cha kitunguu.

"Kutokana na umuhimu wa zao la kitunguu serikali imetupatia Sh. bilioni 38, ambazo zitatumika kujenga miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji. Tunaishukuru serikali chini ya uongozi wa Rais Samia kwa kazi kubwa wanayoifanya hasa kwenye sekta ya kilimo kwa kuwa kilimo ndiyo uti wa mgongo wa taifa letu tangu tulipopata uhuru," alisema.

Pia alisema eneo hilo ni lango kuu la utalii kwa kuwa watalii wanapokwenda kutembelea vivutio vya utalii katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), ni lazima wapitie Karatu.

"Katika Halmashauri ya Karatu kuna hoteli za kitalii zaidi 90, hivyo hoteli zote zinawategemea wakulima kuzalisha chakula cha kuwalisha wageni wanaofika hapa kwa ajili ya kutembelea vivutio vya utalii katika hifadhi zetu," alisema Hokororo.

Alisema halmashauri hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 hali ya ukusanyaji wa mapato inaridhisha kwa kuwa walikasimiwa kukusanya Sh.bilioni 5.5, lakini walivuka lengo kwa kukusanya Sh.bilioni 6.2.

Alisema: "Tumefanya kazi kubwa kwa kushirikiana na timu ya ukusanyaji wa mapato kwa kuwa tumefanikiwa kukusanya zaidi ya Shilingi bilioni moja, kwa lengo tulilokasimiwa na mwaka huu tumepanga kukusanya Sh.bilioni 5.9 na tunatarajia tutavuka lengo na kukusanya zaidi ya kile tulichopangiwa".

# Atiwa mbaroni kwa tuhuma kunyonga mtoto hadi kufa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

JESHI la Polisi Mkoa wa Kilimanjaro linamshikilia mkazi wa Kijiji cha Mahango wilayani Rombo (jina limehifadhiwa) kwa tuhuma za kumuua kwa kumnyonga mtoto Amedeus Laurent (7).

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Mwandamizi wa Polisi (ACP), Simon Maigwa, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema lilitokea Agosti 6 mwaka huu katika Kijiji cha Mahango.

Alisema mama wa mtoto huyo (jina limehifadhiwa) alifika kituoni Agosti 6 baada ya kutomwona mwanawe.

"Mama mzazi wa mtoto huyo alifika katika kituo cha Polisi Agosti 6, 2024 na kutoa taarifa kuwa mtoto wake haonekani nyumbani tangu Agosti 5 majira ya saa 12:00. Tulianza uchunguzi na taarifa za awali zilituonyesha mtuhumiwa alikuwa na mtoto huyo, ingawa alikana na upelelezi unaendelea," alisema.

Alisema Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wananchi walifanikiwa kuupata mwili wa mtoto huyo na mtuhumiwa baada ya kubaini kuonekana kwa mwili alikiri kuhusika na tukio hilo.

Aidha, Kamanda Maigwa, alisema Jeshi la Polisi linakamilisha taratibu nyingine za uchunguzi na mtuhumiwa atafikishwa mahakamani.

Alisema: "Tunatoa onyo kwa watu wote wanaojihusisha matendo ya udhalilishaji, ukatili na mauaji na hatutasita kuchukua hatua kali za kisheria."




Kamanda wa Polisi, Kitengo cha Usalama Barabarani, Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, ASP Leonard Bandola, akitoa elimu na maelekezo kwa madereva na wamiliki wa mabasi ya kubeba wanafunzi juzi alipokagua baadhi ya magari ya shule katika uwanja wa Jitegemee Muheza. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Kamati kuweka msukumo mradi bomba la mafuta

**Na Oscar Assenga,** TANGA

MWENYEKITI wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Oran Njeza, amesema wataendelea kuweka msukumo kwenye mradi wa kimkakati wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), ili kuleta mageuzi ya kiuchumi kwa Watanzania.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati wajumbe wa kamati hiyo walipotembelea na kukagua utekelezaji wa mradi wa EACOP, katika kituo kitakachotumika kupokea, kuhifadhi na kusafirisha mafuta ghafi kutoka Uganda kilichopo Kata ya Chongoleani katika Jiji la Tanga.

Hata hivyo, baada ya kukagua kituo hicho, Njeza, alisema kamati hiyo ambayo inasimamia mipango na uchumi wa nchi imeona mradi wa EACOP una umuhimu kiuchumi.

Aidha, alisema kamati yake itaendelea kuweka mkazo na msukumo katika hatua ya kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati na kuleta manufaa kwa Watanzania.

Vilevile alisema kamati hiyo baada ya kutembelea mradi huo wamejionea maendeleo makubwa na walitumia fursa hiyo kuipongeza serikali kwa mabadiliko ya kiuchumi.

Alisema kuwa serikali imefanikiwa kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ukiwamo wa EACOP ambao unaendana na jinsi dunia inavyokwenda kwa sasa.

Katika hatua nyingine kamati imeitaka Wizara ya Nishati, kuweka kipaumbele cha ujenzi wa mabomba yatakayosafirisha nishati mbalimbali ikiwamo gesi na mafuta.

Wajumbe hao walisema kujengwa kwa mabomba hayo kunatokana na Tanzania kuwa kituo cha usafirishaji wa nishati hizo Afrika.

Pia kamati hiyo imeagiza Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), kuongeza nguvu ya kuutangaza mradi huo ili wananchi wafahamu jinsi serikali inavyoendelea kutekeleza miradi yake.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Burian alisema mradi wa EACOP, utakuwa na manufaa mbalimbali katika mkoa huo ikiwemo kutoa ajira takribani 900, kuongeza mzunguko wa fedha na fursa za biashara.

Kadhalika alisema kituo hicho kitapokea, kuhifadhi na kusafirisha mafuta na kuuza rasilimali ikiwamo saruji na kupata mapato mbalimbali kupitia ushuru.

Dk. Batilda alisema serikali mkoani humo pia imetilia mkazo suala la afya na usalama pahala pa kazi katika miradi mbalimbali na ameipongeza EACOP kwa kutekeleza suala hilo kwa ufanisi.

Alisema katika saa zaidi ya milioni mbili walizofanya kazi hakuna ajali iliyotokea kwenye maeneo yao ya kazi.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dk. James Mataragio, alisema mradi huo utakuwa kielelezo na wa kimkakati kutokana na faida zake.

Alisema faida zitakazopatikana kwenye mradi huo ni pamoja na kuongeza mapato ya nchi kwa kipindi cha ujenzi kwa uendeshaji wa Sh. trilioni 2.3, kutoa ajira kwa Watanzania 7,584 huku ajira hizo zikitarajiwa kuongezeka.

Alisema kampuni 146 za kitanzania zimehusika kutoa huduma mbalimbali kwenye mradi na kunufaika kwa kuongeza kipato kwa kiasi cha Dola za Marekani milioni 246.

Alisema mradi umesababisha kufanyika kwa manunuzi ya Dola za Marekani milioni 462, pamoja na vijana wa kitanzania kupata mafunzo ya teknolojia na ujuzi.

Dk.Matarajio alisema mradi unaendelea vizuri na kwa sasa umefikia asilimia 39.2, huku baadhi ya kazi zikikamilika ni kwa asilimia 100.

Alisema ujenzi wa kiwanda cha kuwekea mabomba ya mfumo wa kuhifadhi joto cha Sojo, umefikia asilimia 90 na katika eneo la Chongoleani mradi umefikia asilimia 40, unataraa kukamilika Juni 2026.





# INEC yaonya udanganyifu uandikishaji wapigakura

**Na Vitus Audax,** MWANZA

TUME Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) imewaonya maofisa wa uandikishaji na uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura kujiepusha na udanganyifu kwa kusimamia kanuni, sheria na miongozo iliyowekwa ili kufanikisha kazi hiyo kwa asilimia 100.

Rai hiyo ilitolewa juzi jijini hapa na Mjumbe wa Bodi ya INEC, Magdalena Rwebangira wakati akihitimisha mafunzo yo ujazaji wa fomu za uandikishwaji na matumizi ya vifaa vya bayometriki.

Magdalena, alisema kila ofisa anatakiwa kuhakikisha anasimama katika kiapo chake kwa kuwa sehemu ya utekelezaji wa majukumu aliyopangiwa katika uboreshaji wa daftari hilo ili kuhakikisha hatua hiyo inafanikiwa.

"Nyinyi mna majukumu na mamlaka makubwa katika maeneo yenu kuhusiana na hatua hii, hivyo mambo yakienda mlama uongozi wenu utatiliwa mashaka na zaidi ya hapo athari zake zitatikisa Taifa," alisisitiza.

Vilevile, aliwataka maofisa hao kutoa kikamilifu mafunzo hayo kwa maofisa uandikishaji wasaidizi ngazi za kata walikopangiwa.

Mwenyekiti wa mafunzo hayo, Emmanuel Shirembi, alisema muhimu kwa washiriki kwa kila mmoja kujengewa uwezo wa kumsaidia kutimiza majukumu yake katika aneo lake.

Shirembi aliahidi kusimamia na kufuata maelekezo ya kisheria ili kudhibiti udanganyifu na kufanikisha majukumu waliyopewa.

Mafunzo hayo yanatolewa kwa maofisa hao wakati Tume hiyo imeanza uboreshaji wa daftari hilo katika baadhi ya maeneo nchini.

Mzunguko wa kwanza ulianza kwa mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora Julai 20 hadi 26, mwaka huu. Wa pili Kagera na Geita ulifanyika kati ya Agosti 5 hadi 11 wakati tatu kwa Mwanza na Shinyanga unatarajia kuanza Agosti 21 hadi 27.



Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa, Godfrey Mnzava, akigawa vyandarua kwa wanawake wajawazito katika Hospitali ya Manispaa ya Shinyanga juzi, alipowasili kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD. **PICHA: MARCO MADUHU**

## EWURA yahamasisha matumizi gesi majumbani

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MENEJA wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Kanda ya Ziwa, George Mhina ameitaka jamii kutambua kuwa matumizi ya kuni na mkaa ni ghali kuliko nishati safi ya gesi.

Mhina aliliambia Nipashe juzi kuwa licha ya kuni na mkaa kuathiri mazingira na afya, ni ghali tofauti na matumizi ya gesi gharama yake kwa mwezi ni kati ya Sh.30,000 hadi 35,000.

Alifafanua kuwa kuni na mkaa, matumizi yake ni zaidi ya Sh. 60,000 kwa mwezi, ambazo jamii ingeweza kunusuru nusu yake kwa kutumia gesi kwa ajili ya kupikia majumbani.

Alisema ili kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kuhifadhi mazingira, jamii inatakiwa kutumia nishati safi na rafiki kwa mazingira ambayo pia itawasaidia kupunguza matumizi.

"Rais (Samia Suluhu Hassan) yupo pamoja na wananchi muda wote, hivi karibuni alizindua mpango mkakati wa miaka 10 (2024-2034) wa kuhimiza nishati safi ya kupikia ukiwa na lengo la kuhakikisha unafikia asilimia 80 ya matumizi ya nishati hiyo katika kipindi hicho," alisema Mhina.

Alisema takwimu zinaonesha wanawake wamekuwa wakipoteza maisha kwa kuvuta hewa chafu inayotokana na moshi wa kuni na mkaa.

Alisema takwimu pia zinaonesha zaidi ya watu milioni 32 upoteza maisha kila mwaka dunia kote.

Alisema vifo hivyo vinachangiwa na madhara ya kuvuta hewa inayotokana na moshi wa kuni na mkaa na kuahidi kuendelea kutoa elimu kwa jamii ili kuhakikisha inabadilika na kuanza kutumia nishati safi.

## Wachangishana kujenga wodi ya mama, mtoto

**Na Ambrose Wantaigwa,** BUTIAMA

WAKAZI wa Kijiji cha Mwibagi Kata ya Kyanyari wilayani hapa Mkoa wa Mara wamechanga zaidi ya Sh. milioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya mama na mtoto katika zahanati ya kijiji hicho.

Wakazi hao walichanga kiasi hicho cha fedha na mabati 330, saruji mifuko 245 na tofali 1,000 katika harambee iliyofanyika hivi karibuni.

Akiendesha harambee hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Butiama, Moses Kaegele, aliwataka wakazi hao kutunza fedha na vifaa vya ujenzi huo na viongozi kuweka utaratibu wa kuanza ujenzi wa wodi hiyo baada ya siku tatu kuanzia siku ya harambee.

Mbunge wa Butiama ambaye ni Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Jumanne Sagini alichangia Sh. milioni 7.5, tofali 1,000 na kumpongeza Diwani wa Kata ya hiyo, Mgingi Mhochi kwa kutafuta wadau wa maendeleo kufanikisha utekelezaji miradi ya maendeleo ya wananchi kwenye maeneo yake.

Sajini, alisema serikali imefanikisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Butiama ili kuwawezesha wananchi kupata huduma karibu na kuwaondolea adha ya kwenda katika wilaya jirani za Bunda na Musoma.

Diwani wa Kata ya hiyo, Mgingi Mhochi aliwashukuru viongozi wa serikali, wadau wa maendeleo na wananchi kwa ushirikiano wanaoendelea kumpatia kukamilisha ujenzi wa jengo hilo ambao baada ya kukamilika, utapunguza gharama za kutafuta matibabu kwa kinamama.

Ili ujenzi wa jengo hilo kukamilika kwa asilimia 100, utagharimu zaidi ya Sh. milioni 156.

## Wanafunzi wasichana wajengewa bweni

**Na Alex Sayi,** MASWA

SHULE ya Sekondari ya Mwagala wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga itaondokana na tatizo la baadhi ya wanafunzi wasichana kuacha masomo na kukithiri kwa utoro baada ya kukamilika kwa ujenzi wa bweni.

Ujenzi wa bweni hilo ambao uliwekewa jiwe la msingi na Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa kwa mwaka huu, Godfrey Mzava hivi karibuni, umegharimu Sh. milioni 163.7.

Akizungumza juzi kuhusu ujenzi wa bweni hilo, Mkuu wa Shule hiyo, Mwalimu Jeremia Masolwa, alisema kabla kulikuwa na wimbi la utoro wa wanafunzi kutokana na umbali wa shule hiyo kutoka kwenye maeneo wanakoishi.

"Shule hii ina wanafunzi 601 kabla ya kujengwa kwa bweni hili watoto wa kike walikuwa wakikatisha masomo kwa sababu ya umbali wa shule na wengine kupata ujauzito, kukamilika kwake itakuwa ni mwarobaini wa hali hiyo,"alisema Masolwa.

Mwanafunzi wa kidato cha pili, Maria Marko, alisema: "Mimi natoka Kijiji cha Gula umbali wa kilomita saba, wengine wanatembea umbali wa zaidi ya kilomita 10 kwenda shuleni na kurudi nyumbani, njiani tunakutana na vikwazo vingi, hivyo bweni hili litatusaidia kupata muda wa kutosha kujisomea."

Mmoja wa wazazi wa wanafunzi wanaosoma shuleni hapo, Mkazi wa Lalago, Njile Ntungwa, alisema bweni hilo litawasaidia watoto wa kike kumaliza masomo yao baada ya kukabiliana na changomoto ya kushawishiwa na wanaume njiani na kupelekea kukatisha masomo yao.

Mkuu wa Wilaya ya Maswa, Aswege Kaminyoge, alisema pamoja na bweni hilo wilaya hiyo ina miradi saba yenye thamani ya Sh. bilioni 4.7 ambayo ilipitiwa na Mwenge, miwili ilizinduliwa, mitatu kuwekewa jiwe la msingi huku miwili ikitembelewa na kukaguliwa.

Nipashe
# TESA
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI
Jumanne Agosti 13, 2024




**REGINA NDLOVU, Gwiji wa sanaa, mijadala mitandaoni kutetea wenye ualbino**


Ukurasa 12

Ukeketaji unavyozidi kuwa suala sugu kwa jamii nyingi


Ukurasa 13

Miaka 0 hadi 8 umri muhimu wa makuzi ya mtoto unavyopuuzwa na wazazi, walezi

ELIMU

**NA MARCO MADUHU, SHINYANGA**

# Ni zamu ya wanaume pekee kupewa somo hili

ATHARI za mila kandamizi na mfumo dume kwenye maendeleo ya wanawake na watoto, zinazungumzwa mno na pengine unaweza kusema kila sikio limesikia.

Hata hivyo, bado hali ni mbaya kwa wanawake kwani wanaendelea kubanwa na mifumo kandamizi iliyopo ndani ya jamii, ili kuubadili upepo, wanaume waanze kufunzwa athari za mifumo kandamizi hiyo.

"Elimu inahitajika zaidi kwa wanaume vijijini, kuhusu umuhimu wa kuachana na mila kandamizi, kunyanyasa na tweza wanawake ili kuimarisha usawa wa kijinsia ili kufikia uwakilishi wa 50/50 kwenye uongozi," anasema.

Diwani wa Viti Maalum Wilaya ya Shinyanga, Zawadi Mwasha, elimu ya kuachana na mifumo kandamizi kwa wanaume vijijini inahitajika.

Anasema mila kandamizi na mfumo dume vinapewa nafasi kubwa, tena ni chanzo cha kukwamisha wanawake vijijini wanapothubutu kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ukiwamo wa kisiasa.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake wa Lyabukande wilayani Shinyanga, Mary Revocatus, anaeleza kuwa vijijini kuna mambo mengi yanayowazuia na wanakumbana navyo, ambavyo ni vikwazo vinavyotokana na mila na mfumo dume iliyopo katika jamii.

Yote hayo yanawakwamisha katika kuwania nafasi za uongozi, licha ya kuhamasishwa kujitokeza kwa wingi kugombea katika chaguzi mbalimbali nchini.

"Katika maeneo ya vijijini mwanaume ndiye mwenye sauti na maamuzi ya kila kitu, ikiwa mume hajaunga mkono azma yako ya kugombea uongozi kisiasa au kushiriki jambo lolote huwezi kuchukua fomu," anasema Mary.



Diwani wa Viti Maalumu, Eunice Magese. **PICHA: MARCO MADUHU**

Diwani wa Viti Maalumu wa Lyabukande Eunice Magese, anasema katika safari yake ya kisiasa bila ya mumewe kumuunga mkono, asingefanikiwa kuwa diwani hadi sasa kutokana na vikwazo vya mila kandamizi na mfumo dume.

Anaeleza kuwa, usaidizi kutoka kwa mumewe ulikuwa muhimu sana katika safari yake ya kisiasa, na pia alikuwa akimpatia fedha za kuendesha kampeni.

"Mume wangu ameniunga mkono sana katika safari yangu ya kisiasa, bila msaada wake ingekuwa vigumu kufanikisha kutokana na ukandamizi," anasema Eunice.

Hata Diwani Zawadi Mwasha, anasema jambo hilo pia naye kwenye safari yake mumewe alimshika mkono.

Mwalimu Upendo Dickson wa Shule ya Msingi Lyabukande, anasema mwanamke anapaswa kujengwa kuwa kiongozi kuanzia ngazi ya familia ili kumpatia ujasiri na hata kuzungumza mbele za watu, lakini kwa maeneo ya vijijini hawapewi nafasi sababu ya mila hivyo wakikua wanaendelea kuwa waoga.

"Tunahijati kuwajenga watoto wetu kujiamini tangu wakiwa wadogo na kuacha kuwathamini watoto wakiume pekee, tuwapatie nafasi mabinti wawe wanashiriki vikao vya familia na kutoa mawazo yao na siyo kuwa watu wa kupewa maagizo tu ili kuwajengea ujasiri mapema," anasema Upendo.

Mzee maarufu wa Lyabukande Peter Amos, anasema mila kandamizi ni kikwazo kikubwa kwa wanawake kugombea nafasi za uongozi, na kwamba mwanawake kimila anapaswa kuongozwa na wanaume na kupewa maagizo na siyo kuwa kiongozi.

"Kimila mwanamke kazi yake ni kumhudumia mwanaume na kupokea maagizo kutoka kwake, akishakuwa kiongozi anabadilika sababu atakuwa na majukumu mengi na kusahau mume. Sasa hapo nilimuoa mke kuwa kiongozi au kunihudumia," anahoji Amos.

Emmanuel Mongo anawashauri wanawake wanaoshika nafasi mbalimbali za uongozi, wafanye ziara za kukutana na kuhamasisha wanawake wengine kwa kuwapa uzoefu na changamoto zake ili kuwatia moyo pamoja na kutoa elimu kwa wanaume ili waache ukandamizi kwa wanawake.

"Mila kandamizi huku vijijini zinawakwamisha kuzungumza kwenye mikutano wa hadhara hawawezi, hivyo ambao wamefanikiwa kwenye uongozi wanapaswa kuzungumza na wenzao ili kuwatia moyo na kuweleza mbinu walizotumia hadi kupata nafasi walizonazo za uongozi," anasema Mongo.

Marco Faida anatoa ushuhuda jinsi wanawake walivyoathiriwa na mila kandamizi pamoja na mfumo dume, ambapo dada yake alimfuata na baadhi ya wazee nyumbani kwake na kumshauri kuwa, katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu 2024 ajitokeze kugombea nafasi ya uongozi.

Anasema baada ya kuelezwa hivyo, dada alimfuata na kumwambia hawezi kuwa kiongozi kwa sababu hana uwezo wa kuongea mbele za wanaume, anaogopa pia ataonekana kama hana nidhamu.

"Nilimtia moyo kwamba watu wamekufuata wanaona unaweza, hivyo kubali tutakuunga mkono lakini nikaona hayupo tayari kabisa," anasema Faida.

**INAENDELEA UK. 13**

ELIMU

**NA SABATO KASIKA**

# Ukeketaji unavyozidi kuwa suala sugu kwa jamii nyingi

• Wanaharakati wapasua vichwa kuelimisha umma



Elimu ikitolewa kwenye kijiwe cha wacheza drafti Kipunguni Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

TAARIFA ya hivi karibuni ya mtandao wa asasi 12 za kupinga ukeketaji nchini inaonesha kuwa, licha ya jitihada zinazofanywa na serikali na wadau kupambana na ukeketaji, bado vitendo hivyo vinaendelea bila uoga.

Anaonya Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni jijini Dar es Salaam, Seleman Bishagazi, alipozungumza na gazeti hili kuhusu mbinu wanazotumia kupambana na vitendo hivyo.

Anasema wameanza kampeni na wataendelea hadi Desemba, mwezi ambao ukeketaji unashamiri wakati wa likizo, na kwa kisingizio kuwa mwaka huu unagawanyika kwa mbili, hivyo umejaa neema.

"Kwa wale wasiojua, Dar es Salaam ukeketaji upo, ingawa kwenye kata yetu ya Kipunguni vitendo hivyo vimepungua, lakini ni muhimu tuendelee kuelimisha umma ili visiongezeke." Anasema.

Anataja kata za jirani ikiwamo ya Msongola kuwa, ukeketaji upo na kwamba walianza kampeni hiyo hivi karibuni, na wanatarajia kufika katika maeneo mengi yenye mkusanyiko.

Anasema wanalenga kufikia masoko, gereji, kwa mama na baba lishe, viwanja vya mipira, stendi za bajaji na bodaboda, vijiwe vya kahawa na vya madalali.

"Lengo letu ni kuijengea jamii uelewa wa kutosha kuhusu madhara ya ukeketaji na pia kuwaelimisha watu kutambua viashiria vya ukatili.

Pia, kuwapa elimu ya afya ya uzazi, kadhalika kuwapa maelezo ili kujua mahali sahihi pa kutoa taarifa za ukatili huo unapotokea kwenye jamii, anasema Bishagazi.

Aidha, watatoa elimu kuhusu ulinzi wa mtoto, madhara ya rushwa ya ngono na umuhimu wa wanaume kushiriki kuzuia ukatili hasa ukeketaji na ukandamizaji wa wanawake.

Mkurugenzi huyo anasema, mwaka unaogawanyika kwa mbili kama huu wa 2024 unachukuliwa kama msimu maalumu wa ukeketaji, kwa maelezo kuwa washiriki wanaamini kuwa ni mwaka wa neema.

"Si kwamba miaka mingine isiyogawanyika kwa mbili hawakeketi, wanafanya hivyo lakini si kwa wingi kama inavyofanyika kwenye mwaka unaogawanyika kwa mbili," anasema.

### WADAU WA KAMPENI

Bishagazi anawataja washiriki wa kampeni hiyo kuwa ni klabu za kupinga ukatili zilizo chini ya kituo hicho, wataalamu wa afya ngazi ya jamii, viongozi wa serikali za mitaa na Diwani wa Kata ya Kipunguni.

Anasema, mkakati huo ni kutekeleza mpango kazi waliokubaliana kwenye vikao vya klabu wa kupita sehemu yoyote yenye mkusanyiko wa watu kutoa elimu hiyo ili kutokomeza ukeketaji katika eneo lao ambayo ni mila yenye athari kiafya.

Diwani wa Kata ya Kipunguni, Steven Mushi, anasema ameungana na kituo hicho katika kampeni hiyo ili kuwafikia vijana, kina mama, wanaume, wazee na watu wenye ulemavu.

"Wazo la kuanzisha kwa kampeni hii lilitokana na klabu za kupinga ukatili ndani ya jamii ambapo viongozi wa Kituo cha Sauti ya Jamii walinishirikisha niwasaidie katika kampeni hii," anasema Mushi.

Diwani anasema, atajitahidi kwa hali na mali kampeni hiyo imfikie kila mwanajamii katika eneo lake ili kufanikisha kuwapo mabadiliko katika jamii.

"Kipunguni imepakana na kata ambazo zinakeketa, kwani baadhi ya wakazi wake wametokea katika mikoa inayoendeleza mila hiyo, hivyo hatuna budi kuendelea kuelimisha umma kuacha vitendo hivyo," anasema.

Anasema, taarifa za mashirika mbalimbali zimekuwa zikionesha jinsi ambavyo ukeketaji bado ni hatari na kwamba wao kwenye Kata ya Kipunguni wameamua kuchukua hatua hizo.

"Kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa linalotetea haki, Usawa wa Wanawake na Wasichana UN, zaidi ya wanawake na wasichana milioni 200 duniani kote wamepitia ukeketaji." Anasema Munisi.

Anasema, shirika hilo linaeleza kuwa, mwaka huu wa 2024, takribani wasichana milioni 4.4 watakuwa katika hatari ya kufanyiwa ukatili huo, ikiwa ni wastani wa zaidi ya kesi 12,000 kila siku.

"Lakini takwimu za demografia ya afya za mwaka 2015 zinaonyesha kuwa, asilimia 10 ya wanawake wenye umri kati ya miaka 15 hadi 49, wamekeketwa hapa Tanzania, huku takwimu za mwaka 2022 zikionesha kuwa, idadi hiyo imepungua kwa asilimia mbili tu ambapo kwa sasa ni asilimia nane ya wanawake wa umri huo wamekeketwa," anasema.

Wakati kata hiyo ikiwa katika kampeni hizo, taarifa zinazotolewa hivi karibuni na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, zinataja mikoa yenye kiwango kikubwa cha ukeketaji ambapo kwa sasa ni Arusha yenye asilimia 43.

Kwa mujibu wa Waziri, mikoa mingine na asilimia zake kwenye mabano ni Manyara (43), Mara (28), Singida (20), Tanga (19), Dodoma (18), Iringa (12) na Morogoro (10).

Pia anautaja Mkoa wa Kilimanjaro kuwa na asilimia tisa, Njombe saba, Pwani tano na Mbeya asilimia tatu, na kwamba wizara inaendelea kutekeleza mkakati wa kupunguza vitendo hivyo kufikia asilimia tano ifikapo mwakani ambao ni ukomo wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.

ELIMU

NA JULIETH MKIRERI, KIBAHA

# Miaka 0 hadi 8 umri muhimu wa makuzi ya mtoto unavyopuuzwa na wazazi, walezi

SHIRIKA la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) katika ripoti yake ya Juni mwaka huu, inaeleza kwamba watoto karibu milioni 400 wanakabiliwa na ukatili wa kimwili na kisaikolojia nyumbani, ambapo kati yao asilimia 60 wapo chini ya umri wa miaka mitano.

Takwimu hizo zilizokusanywa kutoka katika mataifa 100 kuanzia mwaka 2010 hadi 2023 zinajumuisha aina zote za ukatili ikiwamo adhabu za kimwili na unyanyasaji wa kisaikolojia.

UNICEF inakumbusha kuwa, ukatili wa kisaikolojia unajumuisha maneno ya kubezwa, kupewa majina yanayochukiza kwenye jamii, wakati ukatili wa kimwili ni pamoja na matendo yote yanayosababisha maumivu mwilini au usumbufu, bila majeraha.

Akizungumzia kwa upande wa bara la Afrika, Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Pwani, Edna Kataraiya, anabainisha kuwa robo tatu ya watoto walio chini ya miaka mitano wanaoishi Kusini mwa Jangwa la Sahara wapo kwenye hatari ya kutofikia hatua zao za ukuaji.

Ni masuala yanayoibuka wakati wa mkutano wa tathmini ya kutekeleza Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi na Makuzi ya Maendeleo ya Awali ya Mtoto, unaofanyika Kibaha mkoani Pwani.

Anasema takwimu zinaonyesha kwamba, dunia ina watoto milioni 250 wenye umri wa chini ya miaka mitano na robo tatu ya idadi hiyo ni sawa na asilimia 66 ya watoto hao wanapatikana Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Pia, Edna anasema zipo changamoto katika uwekezaji wa malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto kuanzia miaka sifuri hadi nane kutopewa uzito unaostahili badala yake msisitizo imewekwa kwenye kupunguza vifo.

Kwa mujibu wa maelezo yake, kipindi hicho ni wakati muhimu wa kuboresha maendeleo ya binadamu na hivyo kupata mtaji bora wa rasilimali watu wenye tija kitaifa.



Watoto wa umri wa chini ya miaka minane wakiwa kwenye mazingira magumu mtaani. **PICHA: MTANDAO**

Ili Programu hiyo kufikia malengo yake katika Mkoa wa Pwani, anaziagiza Halmashauri za Mkoa huo kutenga bajeti kwa ajili ya kutekeleza yaliyolengwa kufanyika kwenye maeneo yao.

Mratibu wa masuala ya Malezi na Makuzi na Maendeleo ya awali ya mtoto kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknilojia, Dk. Hawa Selemani, anaeleza kwamba pamoja na serikali kuwekeza zaidi kwenye eneo hilo bado kuna vikwazo.

"Kuna changamoto kwa watoto tunaowalenga, kuna walioko mitaani, ukatili na unyanyasaji havijaisha na hii inatufanya sasa tufikirie kuwa na mfumo wa pamoja wa kufuatilia yale tunayoyafundisha kwenye jamii," anasema.

Kadhalika ni vyema kufuatilia kwenye vituo vya malezi ya watoto ili kupata uhakika kama wanatoa huduma kama kanuni zinavyoelekeza na kama wanaenda tofauti wapewe elimu itakayo kwa wawezeshaji kwenda sawa na malengo, anasema Dk. Hawa.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Pwani, Lidya Mafole anasema kuwa, kwa sasa mkoa una vituo 730 vya malezi ya watoto na tunawafuatilia na kuhimiza kufuata taratibu na kanuni za kisheria zilizowekwa kwenye malezi yao.

Mshiriki Uzima Justine, kutoka Taasisi ya Tuwalee Child Organization (TUCO) iliyopo Chalinze anasema kila taasisi kabla ya kutekeleza mradi ifanye utafiti kwa kukusanya takwimu kupitia viongozi wa serikali kwenye maeneo yao.

"Zipo taasisi zinazofanya miradi ya watoto lakini bado matatizo yanaendelea kuongezeka kwa mfano suala la ukatili, hivyo kutokana na hali hii ni vyema kufikiria ni kwa nini matukio hayo yanaongezeka wakati taasisi nyingi zimejikita kwenye kutekeleza miradi? Ndipo unapokuja umuhimu wa kuanza na utafiti," anasema Justine.

Kadhalika anaomba Kamati za Ulinzi na Usalama kwenye wilaya kuwa na ajenda ya watoto kwenye vikao vyao zinazoanzia kwenye kamati za ngazi za tarafa, kata, vijiji na vitongoji au mtaa.

Pia, anashauri kuzingatia idadi ya watoto kwenye vyumba vya madarasa sambamba na kutumia miongozo iliyoandaliwa na serikali itakayosaidia katika kuimarisha malezi na makuzi bora ya watoto.

Mwakilishi wa Shirika la Tecden, Christopher Peter, akizungumzia suala la malezi ya watoto katika jamii kwenye mkutano huo, anaitaka jamii kuzingatia zaidi ulinzi, usalama, haki na mahitaji ya watoto ili wakue salama.

Programu hiyo, katika Mkoa wa Pwani inatekelezwa na serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Anjita, Shirika la Tecden, Children in Crossfire na Umoja wa Vilabu vya Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC)

Peter anakumbusha kuwa, serikali inataka kila mwanaume aambatane na mwenza wake kwenda kliniki kulinda afya ya mjamzito na mtoto jambo ambalo litaleta ushirikiano chanya katika masuala ya malezi na makuzi ya mtoto.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

Washiriki wa mkutano huo wanasisitiza kuwa, ili kuwa na malezi bora katika kipindi cha miaka sufuri hadi minane katika ukuaji wa mtoto, ni muda ambao ubongo unakua kwa kasi na unachukua taarifa nyingi za mazingira mbalimbali wanapoishi.

Kwa hivyo, malezi na makuzi anayopata yanaweza kuwa na athari mbaya au bora katika maisha yake yote.

Aidha, yapo madhara ambayo yanaweza kutokea endapo mzazi au mlezi hatamzingatia mtoto ipasavyo katika kipindi hicho. Madhara hayo ni pamoja na watoto ambao hawapati vichocheo vya kutosha kiakili wanaweza kuwa na shida katika kujifunza, kutatua matatizo yanayowakabili na kukosa kuzingatia maelekezo.

Aidha, malezi mabaya yanaweza kusababisha watoto kuwa na matatizo ya kihisia kama vile wasiwasi, unyogovu na ukosefu wa kujithamini.

Watoto ambao wanakua katika mazingira yenye ukatili au kupuuzwa wanaweza kuwa na tabia za ujeuri, utovu wa nidhamu, na uasi na wale ambao hawapati lishe bora na huduma za afya hawawezi kukua kikamilifu.

**UBONGO IMARA**

Pia, kipindi hicho ni muda ambao ubongo wa mtoto unaundwa, unakuwa na miunganisho mipya, kila sekunde huunda msingi wa jinsi mtoto atakavyofikiria, kujifunza na kujichanganya na wenzake.

Watoto wanahitaji kuhisi kuwa, wanapendwa na kutunzwa; na katika kipindi hiki wazazi na walezi wazungumze na watoto mara kwa mara na kuwasikiliza kwa makini huku nidhamu ikipewa kipaumbele, upendo na maonyo ya kuwaelimisha.

Pia wazazi na walezi wanapaswa kuchochea akili za watoto wao kwa kuwasoma, kucheza nao, na kuwapeleka kwenye shughuli mbalimbali za kujifunza na hiyo itaimarisha malezi mazuri kwa watoto wao kukua na kuwa watu wazima wenye afya bora na furaha.

**HALI HALISI**

Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2022 idadi ya watoto wenye umri sifuri hadi miaka minane nchini ni milioni 16.6 sawa na asilimia 27 ya Watanzania Bara.

Katika idadi hiyo asilimia 47 ya watoto wenye umri kati ya miaka miwili hadi mitano wanaoishi na mama zao wanaelezwa kuwa kwenye muelekeo sahihi wa ukuaji timilifu katika maeneo ya afya kujifunza na kihisia.

Hayo ni kwa mujibu wa ripoti ya utafiti wa afya ya uzazi na mtoto na viashiria vya malaria ya mwaka 2022 kutoka Ofisi ya Takwimu ya Taifa na kwamba asilimia 53 ya watoto wa umri huo wanatajwa kwamba hawako kwenye mwelekeo sahihi wa ukuaji timilifu.

Kwa vigezo hivyo ni lazima kufanya kazi ya ziada na kubadilisha changamoto za watoto ili Tanzania inapoelekea kwenye kuandaa dira ya 2050 iwe na watoto bora kwa maendeleo ya kizazi cha sasa na kijacho.

# NI ZAMU YA WANAUME PEKEE KUPEWA SOMO HILI

**INATOKA UK.11**

Ofisa Tathimini na Ufuatiliaji kutoka Shirika la Kiraia linaloshughulikia maendeleo ya wanawake (WEADO), John Eddy, anasema kwamba shirika hilo linaendesha mdahalo wa kujadili vikwazo vya kijamii vya kimila ambavyo vinakwamisha safari ya mwanamake kiuongozi.

Anasema mdahalo huo unalenga kuondoa mila kandamizi, pamoja na kuhamasisha wanawake kugombea nafasi za uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwakani ili kufikia usawa wa kijinsia katika nafasi za uongozi.

"Jitihada zaidi zinahitajika ili kubadili mitazamo iliyopo ndani ya jamii, kwa kuondoa mila kandamizi na mifumo dume ili tufikie 50 kwa 50 katika nafasi za uongozi," anasema John.

Msimamizi wa Uchaguzi Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Osca Lupavila, anasema katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, kati ya kata 26 wilayani humo ni kata moja tu ambayo mwanamke alishinda nafasi ya uongozi.

Msimamizi wa uchaguzi Manispaa ya Shinyanga Charles Kafulila, anasema bado wanawake wanahitaji hamasa kugombea nafasi za uongozi, na kwamba katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2019, wanawake walishinda viti sita tu kati ya mitaa 55, na vitongoji 84 walishinda viti nane tu.

Uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kati ya kata 17, wanawake walioshinda nafasi ya udiwani ni wawili tu kutoka Kata ya Kitangili na Ndala.

Hali hii inaonesha kuwa, licha ya juhudi na mipango ya kuhamasisha usawa wa kijinsia, wanawake bado wanakabiliwa na vikwazo vikubwa katika kujitokeza na kushika nafasi mbalimbali za uongozi hivyo elimu bado inahitaji katika jamii.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# REGINA NDLOVU

# Gwiji wa sanaa, mijadala mitandaoni kutetea wenye ualbino

KUFIKIA Aprili 2018, ripoti za Wadau wa Kutetea Haki za Binadamu na Vyombo vya Umoja wa Mataifa, vinataja kuwa, mauaji 200 na mashambulizi zaidi ya 500 kwa watu wenye ualbino yanaripotiwa Afrika.

Ni katika mataifa 27 ya Afrika Kusini ya Jangwa la Sahara, Tanzania ikiwamo.

Yote hayo ni kutokana na imani potofu iliyoko maeneo ya Afrika kwamba viungo vya albino vinaleta utajiri, nguvu za kujamiiana na pia ni tiba ya maradhi kama VVU.

Viungo vyao hutafutwa kwa sababu kama hizo

Tanzania, inaripotiwa kuwa takribani wenye ulemavu wa ngozi 75 waliuawa kati ya mwaka 2,000 hadi 2016.

Pia zipo ripoti za mauaji ya wenye ulemavu wa ngozi Afrika Kusini, ingawa uhalifu huo si mwingi kama ilivyo Malawi, Tanzania na Burundi. Februari mwaka jana, mahakama ya Afrika Kusini ilimhukumu mganga wa kienyeji kufungwa maisha kwa kumuua albino mwanamke mwenye miaka 20.

Katika kukabiliana na uhalifu huo, unaohusishwa na ushirikina, Regina Mary Ndlovu (34), raia wa Zambia anayeishi na ualbino, anaendeleza harakati mitandaoni kupinga ukatili huo.

Anasema amekuwa kwa shida katika utoto wake, kwa kuwa hakuna aliyeelewa ualbino ulikuwa nini wakati huo, alipozaliwa.

Wapo waliodhani mama yake alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Mzungu, hivyo baba yake aliwatelekeza , lakini baadaye wakapatanishwa, anasema, inaandika BBC.

Akiwa mtaani na popote watoto wengine mara nyingi walimdhihaki na kumwita majina, kana kwamba wanamwogopa.

Tabia hiyo iliendelea hata shuleni, huku hata mwalimu wake shule ya msingi akisema hastahili kuwa darasani, kutokana na matatizo ya macho, anasema.

Tatizo hilo liliendelea hadi sekondari walimu wakimrusha kwenda madarasa mengine



ingawa hakujua kusoma na kuandika, kisa kumkwepa.

Alinyanyaswa kingono na kimwili akiwa na miaka nane na rafiki wa familia yao. Kisha akiwa katika shule binafsi nchini Zambia, alinyanyaswa kiakili na kimwili na mwalimu.

Simulizi ya Regina anayeishi na ualibino, inasema, alianza kunyanyaswa kingono na rafiki wa familia yao akiwa na miaka nane na kwamba haikuwa mara ya kwanza wala ya mwisho.

Anasema mambo hayo yalifanyika Ennerdale, Afrika Kusini, na rafiki huyo wa familia alikuwa akitumia kisingizio cha kuwatembelea wazazi wa Regina na kumnyanyasa mara kwa mara miaka mingi.

Hakuwa yeye pekee, anaiambia BBC kuwa, amekuwa akikabiliwa na kushambuliwa kwa matukio yaliyokuwa ya kingono na yasiyo ya kingono kwa miaka mingi.

Regina anasema mashambulio yanamlenga kwa sababu tu alizaliwa na ualbino.

Kuwa albino kunatokana na kuathiriwa kwa michakato ya kimbaumbile ya kuzalisha melanin, ambayo hutengeneza rangi ya ngozi ya mwili.

Wanaomshambulia wana imani potofu kwamba kumbaka anayeishi na ualbino kunamzuia kupata magonjwa, Regina anaelezea, kuwa chanzo cha kumdhalilisha huko.

Anasema wazo hili ni moja ya hadithi nyingi za hatari zinazowazunguka watu wanaoishi na ualbino.

Leo baada ya miaka mingi ya kupambana na msongo wa mawazo, anabadilisha maisha yake ni mwigizaji.

Anafanya juhudi zote kutetea uelewa bora wa hali za watu wanaoishi na ualbino na kuwaona kuwa ni wa kawaida badala ya kuwafanyia uhalifu.

Regina anasema licha ya kujifunza kusoma na kuandika miaka 10 iliyopita akiwa na umri wa miaka 24, pia ameandika na kuigiza katika mchezo wake mwenyewe kuhusu ualbino na maisha aliyopitia yeye mwenyewe.

Mama huyu aliyejifungua karibuni anataka kufanikisha na kumaliza manyanyaso kwa wengine wenye ualibino, wasipitie kile alichokiona na kuteswa kwenye maisha yao.

Anapingana na kukabili hadithi zinazozunguka hali hiyo ya kuishi na ualbino.

Anasema wengine wanaamini kuwa, nywele nyeupe za albino zinaweza kuleta utajiri mkubwa, wakati wengine wakiamini dhana potofu zaidi ikiwa ni pamoja na kufanya ngono na mtu mwenye hali hiyo kunaweza kuponya magonjwa kama VVU na UKIMWI.

Kuna maelezo kuwa kuzuka kwa COVID-19, kumekuwa na uvumi wa uongo kwamba mwenye ualbino anaweza kuponya corona pia, inasema BBC.

Watu wanaoishi na ualbino wanatekwa na kuuawa kwa sababu ya imani potofu kwamba viungo vyao vya mwili vina nguvu, hata hivyo ni ushirikina na hakuna ukweli.

**KUONDOKA ZAMBIA**

Regina alihamia Afrika Kusini baada ya kifo cha baba yake, alipokuwa na umri wa miaka 12. Anasema wakati huo alikuwa anajidharau na kujichukia.

Anasema alijaribu mara 11 kujiua. Sasa ni msanii anaangalia harakati za kutetea watu wenye ualbino. Amefanya kazi ya uanaharakati na onyesho lake moja la wanawake, ambalo ni kuhusu Mary mwenye umri wa miaka 8 hadi mwenye miaka 25.

**KUISHI UHALISIA**

Regina ni mwanzilishi mwenza na mtangazaji wa kipindi cha mazungumzo ya mtandaoni, My Voice Albinism the new Era, yanayoweza kutafsiriwa kama 'sauti yangu ualbino katika zama mpya'.

Regina anashiriki katika michezo ya kuigiza, sinema na tamthilia kunakomaanisha maana halisi au kila kitu kwenye maisha yake.

Anaonyesha maisha yake kwa sababu kupitia uigizaji wake watu wanafundishwa ukweli kuhusu ualbino. Anatumia jukwaa hilo kusimulia hadithi za kweli. Inachofanya jukwaani ni maelezo ya namna alivyonyanyaswa kwa muda mrefu pia, kupitia mateso, ubaguzi, kubezwa na katika hali hiyo hakuwa na sauti ya kujitetea.

Regina anasema kushirikishwa katika michezo ya kuigiza, kupanda majukwaani na kuzungumzia hali ya ualbino kumemfundisha kuwa hakuna haja ya kupigana bali ni kuongeza juhudi zaidi kuwaelimisha watu kwamba mwenye kuishi na ualbino ana utu sawa na binadamu wengine.

Anahamasisha upendo na heshima kwa binadamu wote bila kujali maumbile yao.



Regina Ndlovu. **PICHA: MTANDAO**



## Makatibu TCS wakabidhiwa magari

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, amekabidhi magari 10 kwa makatibu wasaidizi wa wilaya wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na kuonya yasitumike kwa anasa.

Mchengerwa alikabidhi magari hayo juzi jijini hapa kwa halmashauri 10 nchini.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi magari hayo, aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri kufuatilia utendaji kazi ili kuhakikisha yanafanya kazi iliyokusudiwa.

"Magari haya naomba niwahakikishie kuwa si anasa bali mmepewa kama vitendea kazi ili muweze kuwafikia walimu popote walipo kwenye maeneo yenu, kuwasikiliza, kutatua kero na changamoto zao na kuwapa ushauri nasaha pale inapolazimika," alisema waziri huyo na kuongeza kuwa:

"Serikali haipendi kuona au kusikia walimu wananyanyaswa au kufanyiwa vitendo vyovyote vinavyoashiria ukatili ambavyo vinaweza kuwasababishia kushindwa kutekeleza majukumu yao, bali inataka kuwaona wakifanya kazi kwa furaha, amani na utulivu wakati wote."

Alisema serikali inatambua changamoto ya upungufu wa vitendea kazi kwa zaidi ya makatibu wasaidizi 139 na imeanza na halmashauri hizo 10 na kwamba baadaye itaendelea kwa nyingine lengo ni maeneo yote kuwa na vitendea kazi.

Kwa upande mwingine, aliwataka waliokabidhiwa magari hayo kuyatumia kwa malengo yaliyokusudiwa na kuyatunza ili yaweze kudumu na kutumika kwa muda mrefu kuboresha utendaji kazi wa walimu.

"Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, imeshatoa magari 394 kwenda kwa makatibu wasaidizi na divisheni ya elimu hao nchini," alisema.

Awali akitoa taarifa kuhusu ununuzi wa magari hayo, Naibu katibu Mkuu TAMISEMI anayeshughulikia elimu, Charles Msonde, alisema umegharimu Sh. bilioni 2.1 kupitia mradi wa kuboresha elimu ya awali na msingi (bust) wenye thamani ya Sh. trilioni 1.15.

# PSSSF, WCF kuendesha kiwanda cha chai Mponde

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imekabidhi uendeshaji wa Kiwanda cha Chai Mponde kwa wanahisa wapya, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Mfuko wa Fidia kwa Watumishi wa Umma (WCF) ili kukuza uzalishaji wa chai nchini.

PSSSF na WCF watamiliki hisa za kiwanda hicho kwa asilimia 84 na Ofisi ya Msajili wa Hazina 16.

Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu, alisema hayo juzi jijini hapa wakati wa hafla ya utiaji saini nyaraka za makabidhiano na mkataba wa wanahisa wa kiwanda hicho kilichoko Wilaya ya Lushoto mkoani Tanga.

Kwa mujibu wa Mchechu, serikali imekuwa ikifanya kazi kubwa katika kuhakikisha uzalishaji wa mazao ya chakula na yale ya biashara unaimarishwa nchini.

Alisema chai imekuwa ni moja ya mazao muhimu na tegemeo katika uchumi wa nchi, lakini siku za hivi karibuni uzalishaji wa zao hilo umeshuka na kupelekea serikali kupitia ofisi yake, kuanza kutafuta njia za kuboresha ikiwa ni pamoja na kufanya uendelezaji wa kiwanda hicho.

"Kutokana na umuhimu wa kilimo cha chai nchini, PSSSF na WCF na Msajili wa Hazina tuliamua kuwekeza katika zao la chai," alisema Mchechu.

Alisema uwekezaji katika mradi huo mpaka sasa umegharimu kiasi cha Sh. bilioni 2.50 na kukamilika kwake kutahitaji Sh. bilioni 4.05 ili kuhakikisha wakulima wa maeneo husika wananufaika na uwekezaji huo wa serikali.

"Uendeshaji wa kiwanda hiki unatarajiwa kuwa na manufaa makubwa kwa kiwanda na Uchumi wa Taifa. Pamoja na mambo mengine kiwanda kinatarajia kuleta manufaa ikiwamo kuongeza amana ya kiwanda kutoka Sh. milioni 790 mpaka Sh. bilioni 4.84 pamoja na kuimarika kwa mtaji na kuvutia wawekezaji," alisema.

Pia alisema kufufua shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuinua zao la chai ambalo kwa sasa linaendelea kudorora katika wilaya za Lushoto na Korogwe, kuongeza mapato ya serikali kupitia kodi na tozo mbalimbali.

Alisema, kwa ujumla zao la chai limekuwa likiingizia nchi wastani wa Dola za Marekani milioni 45 kwa mwaka na kuajiri watu takribani 50,000, na ajira zisizo za moja kwa moja, takribani watu 2,000,000.

"Ofisi ya Msajili wa Hazina inaielekeza Kampuni ya Mponde kusimamia misingi ya kibiashara yenye kuleta usawia na kukuza ufanisi wake kiutendaji.

"Hii ni sambamba na kutumia wataalamu walio katika kampuni hiyo kushauri ipasavyo na kuleta tija katika uzalishaji wa chai. Aidha, Kampuni inaelekezwa kutafuta masoko ya ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuwa na uzalishaji na biashara endelevu katika soko," alisema.

Alisema ofisi yake itaendelea kufuatilia uwekezaji wake kwenye kiwanda hicho na kuonya kuwa haitasita kuchukua hatua haraka pale itakapoona uwekezaji wake hauna tija.

Mkurugenzi wa usimamizi, utendaji, ufuatiliaji na tathmini mashirika yasiyofanya biashara Ofisi ya Msajili wa Hazina, Emmanuel Luvanda, alisema Mponde kilianzishiwa mwaka 1973 na Mamlaka ya Chai Tanzania kupitia Sheria ya Chai (Tea Ordinance No. 8 of 1968) ambayo iliipa mamlaka hiyo majukumu ya kuendeleza, kusindika na kusimamia tasnia ya chai nchini.

Luvanda, alisema uanzishwaji wa kiwanda hicho ulitokana na jitihada za serikali za kuendeleza zao la chai na kuchochea shughuli za kiuchumi katika wilaya za Lushoto na Korogwe ambako ndio zao kuu la biashara.

Alisema kutokana na usimamizi usiokuwa mzuri wa mamlaka uliosababisha kushuka kwa uzalishaji, serikali iliamua kiwanda hicho kibinafsishwe.

Alisema serikali kupitia iliyokuwa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC), ilibinafsisha kiwanda cha Chai cha Mponde mwaka 1999 kwa Umoja wa Wakulima Wadogo wa Chai uliofahamika kwa jina la Usambara Tea Growers Association (UTEGA).



Baadhi ya vijana kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini wakishiriki maadhimisho ya Wiki ya Vijana Kimataifa yanayoendelea jijini Dodoma jana, maadhimisho hayo yalianza Agosti 10 na kilele chake ni leo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Watoto milioni tatu nchini wana utapiamlo

**Na Gloria Maganza,** DODOMA

WATOTO wanaokadiriwa kufikia milioni tatu nchini wanakabiliwa na udumavu kutokana na lishe duni.

Takwimu hizo zilitolewa jana jijini hapa wakati wa uzinduzi wa mradi wa kuimarisha usalama wa chakula kwa kaya za wakulima wadogo 168,000 katika mikoa ya Rukwa, Songwe, Dodoma, Manyara na Singida ili kukabiliana na utapiamlo kwa watoto unaotokana na ukosefu wa lishe bora.

Lengo la kuzinduliwa kwa mradi huo ni kukabiliana na uhaba wa chakula, utapiamlo na kupunguza idadi ya watoto hao chini ya miaka mitano wanaokabiliwa na udumavu nchini hususani Nyanda za Juu Kusini ambako upo kwa asilimia 46.2.

Shirika la Maendeleo la SNV Netherlands kwa kushirikiana na Farm Africa wamezindua mradi huo wa miaka mitano wa kuwawezesha wakulima wadogo kwa usalama wa Chakula na Ustahimilivu wa Tabianchi (NOURISH Tanzania).

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Dk. Hussein Mohamed Omar, alizindua mradi huo ulioshirikisha wadau wengine wa kilimo na lishe, sekta binafsi, vyuo vikuu na washirika wa maendeleo.

"Mbinu ya kampeni ya kubadili tabia itakayofanywa na mradi wa NOURISH kupitia wahudumu wa ngazi ya jamii na watu wenye ushawishi kutoa elimu kuhusu lishe katika kaya itasaidia sana kuinua lishe bora na afya njema.

"Sanjari na hayo, uimarishaji wa mahusiano baina ya wakulima, waandaaji pamoja na masoko utapunguza hasara za mazao baada ya mavuno, kupelekea uwapo wa chakula bora na wakulima kuwa na hakika kuwa mazao yatawafikia watumiaji," alisema Omar.

Mkurugenzi Mkazi wa SNV, Michael Mcgrath, alisema:

"Mradi wa NOURISH utashirikiana na wadau wa kilimo kama vile watoa huduma za ugani, wazalishaji wa mbegu, kampuni za teknolojia na wadau wengine muhimu ili kuongeza maarifa na matumizi ya mbinu na teknolojia za kilimo zinazohimili mabadiliko ya tabianchi.

"Hii inalingana na mkakati wa kitaifa wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi wa Serikali ya Tanzania (2022-2026) na nia ya Kitaifa (2021) ambayo inazingatia sekta ya kilimo kwa kuzingatia mabadiliko na ustahimilivu wa tabia nchi kupitia aina za mazao himilivu, huduma bora za ugani, kukuza mazoea ya kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi na kupunguza hasara baada ya mavuno - yote haya yatakua kipaumbele cha mradi wa NOURISH."

Mbali na SNV na Farm Africa, mradi wa NOURISH utatekelezwa pia kwa kushirikiana na T-MARC, RECODA na MIICO.





# TAKUKURU yakaa mguu sawa kuelekea uchaguzi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya, imeanza mikakati ya kukabiliana na vitendo vya rushwa kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka huu na Uchaguzi Mkuu wa mwakani.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, Maghela Ndimbo, alisema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya taasisi hiyo ikiwamo utendaji kazi wa miezi mitatu iliyopita.

Alisema taasisi hiyo imeshaanza kutoa elimu kwa wadau mbalimbali wa uchaguzi kuhusu madhara ya rushwa wakati wa uchaguzi na namna ya kuepuka vitendo hivyo, ambavyo kwa mujibu wa sheria ni haramu.

Alisema watatumia programu ya TAKUKURU Rafiki kufikisha elimu kwa wadau wakiwamo waandishi wa habari ili na wao washiriki kutoa elimu kwa wananchi na kuripoti vitendo hivyo wakati wa uchaguzi na wakati wa shughuli zingine.

Alisema watu wote watakaobainika wakishiriki vitendo vya rushwa wakati wa uchaguzi watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria za nchi na hivyo akawataka watu wote wenye nia ya kugombea nafasi mbalimbali kuepuka kushiriki vitendo hivyo.

"Elimu ya madhara ya rushwa kwenye uchaguzi imeshatolewa na itaendelea kutolewa kupitia programu yetu ya TAKUKURU Rafiki, hii ni programu ambayo inaweka urafiki wa karibu kati ya taasisi yetu na wananchi na inatusaidia kupata taarifa haraka," alisema Ndimbo.

Aliwataka wananchi kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa kupiga namba ya bure ya taasisi hiyo ambayo ni 113 na kwamba taarifa hizo watazifuatilia ili kuubaini ukweli.

Katika hatua nyingine Ndimbo alisema katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita walifuatilia utekelezaji wa miradi 27 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 150.8 ambayo ni ya sekta ya elimu, maji, umwagiliaji na barabara.

Alisema katika ufuatiliaji huo walibaini mradi mmoja ambao ni wa ujenzi wa Shule ya Wasichana iitwayo Kakao Girls ya wilayani Kyela ilikuwa na dosari kwenye manunuzi ya zaidi ya Sh. milioni 60 akidai kuwa hayakufuata utaratibu.

Alisema walibaini kuwa wajumbe wa kamati za manunuzi na mapokezi ambao ni wanakijiji hawana uelewa juu ya taratibu za manunuzi ya vifaa vya ujenzi kwenye miradi ya umma.

Alisema walibaini kuwa kwenye ununuzi wa vifaa hivyo kulikuwa hakuna ubadhirifu isipokuwa kulikuwa na tatizo kwenye utunzaji wa nyaraka za ununuzi wa vifaa hivyo.



Meza zikiwa tupu katika Soko la Kinyerezi jijini Dar es Salaam juzi, kutokana na wafanyabiashara kulikimbia kwa sababu hakuna wateja. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Wafanyabiashara Soko la Ndanto kufungiwa taa

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Patrick Mwalunenge, ameahidi kufunga taa eneo la Soko la Ndanto katika Halmashauri ya Rungwe ili kuwasaidia wajasiriamali wa eneo hilo kufanya shughuli zao usiku na mchana.

Aidha, ameahidi kuwawezesha vijana 50 mbolea na mbegu ili kuwaunga mkono kwenye kilimo cha viazi mviringo msimu ujao kwa lengo la kuimarisha uchumi wao na kujiinua kiuchumi.

Aliwataka vijana wa kata hiyo kuacha vurugu na badala yake waendelee kufanya shughuli zao za kiuchumi ikiwamo kilimo na biashara ili kujiletea maendeleo pamoja na kuvutia wawekezaji ambao watasaidia kuongeza uzalishaji.

"Tujitahidi kudumisha amani ili eneo letu liendelee na sifa nzuri, ndio maana nimeamua sasa kuwawezesha vijana 50 kupata mbolea na mbegu ili mlime kwa wingi na kukuza kipato chenu," alisema Mwalunenge.

Vilevile aliahidi kuwaunga mkono wananchi wa kata hiyo kwenye ujenzi wa kituo cha polisi ili kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama katika eneo hilo.

Baadhi ya wakazi wa kata hiyo waliiomba serikali kuwasaidia kuboresha miundombinu ya barabara katika eneo hilo ili kuwarahisishia usafirishaji wa mazao mbalimbali ikiwamo viazi ambavyo ndio zao kuu wanalozalisha.

Mmoja wa wananchi hao, Juhudi Mwambenja alisema wakati wa masika huwa wanashindwa kusafirisha viazi na mbolea kutoka mashambani kwenda sokoni hali ambayo inazorotesha uzalishaji.

Alisema kutokana na hali hiyo wamekuwa wakitumia gharama kubwa kusafirisha mazao kutoka kwenye mashamba kwenda barabarani kwa kuwatafuta vibarua wa kujitwisha kichwani.

# Wakazi vijiji 10 waomba kujengewa malambo

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

WANANCHI 34,000 kutoka vijiji 10 vya kata ya Lubonde, Lugarawa na Mlangali wilayani Ludewa Mkoa wa Njombe wameiomba serikali kuwajengea malambo ya kunyweshea mifugo, ili kunusuru vyanzo vya maji ambavyo vimekuwa vikitumiwa na wafugaji.

Walitoa ombi hilo juzi katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kijiji cha Mlangali ambao umeratibiwa na shirika lisilokuwa la kiserikali la Mladea chini ya ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (UNDP).

Walisema endapo malambo hayo yatajengwa yatasaidia pia wananchi kuondoka na tatizo la magonjwa ya tumbo na kuhara ambayo yanasababishwa na kunywa maji pamoja na mifugo.

Mmoja wa wananchi hao akiwamo, Philipo Kayombo alisema dhamira yao ni kutunza mazingira ni vema wafugaji wakatengewa eneo lao ili kunywesha mifugo.

"Kuna watu wanamifugo lakini maji ni tatizo hivyo wanafuata huko huko mtoni ambako wananchi wanatumizi maji hayo kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, hivyo tunaomba kama bajeti itapitikana tuwatengee sehemu kama walivyofanya kule kijiji cha Msomela mkoani Tanga," alisema Kayombo.

Naye Cassiana Msemwa alisema ujenzi wa malambo ni miongoni mwa suluhisho la kuondokana na migogoro baina ya wakulima na wafugaji pamoja na kuhifadhi wa vyanzo vya maji.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mlangali, Mathayo Msigwa, alisema kilio cha wananchi ni kuhakikisha kunapatikana eneo kwa ajili ya kunyweshea mifugo maji.

Ofisa Mazingira Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Lucas Makonope, alisema shughuli za kibinadamu ikiwamo kufyatua tofali na kuingiza mifugo kunasababisha kuchafua vyanzo vya maji na kuviharibu.

"Maji yanachafuka kutokana na mmomonyoko wa udongo unaosababishwa na mtikisiko wa wanyama kwa sababu udongo unaoingia kwenye chanzo na udongo ukishajaa inamaana kina cha maji kinapungua na kupelekea kukauka kabisa, " alisema Mkonope.

Alisema viongozi wa vijiji hivyo wanapaswa kukubaliana ili kutambua eneo moja hasa katika vijiji vyenye matumizi bora ya ardhi ambalo litafaa kwa ajili ya kunyweshea maji mifugo kwa kipindi ambacho serikali inajipanga ili kuweza kutatua tatizo la kujenga malambo.



## ‘Safisheni mazingira msipate magonjwa ya mlipuko’

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANANCHI wametakiwa kusafisha mazingira ili kujikinga na magonjwa ya mlipuko ikiwamo kipindupindu na matumbo ya kuharisha.

Wito huo umetolewa na Msimamizi mkúu wa shughuli za usafi katika Baraza la Manispaa Wilaya ya Magharibi B Unguja, Mohammed Said Abdalla, wakati wa usafi.

Alisema jukumu la kufanya usafi linamgusa kila mtu, hivyo aliwataka wananchi kuachana na dhana potofu ya kuwa jukumu la kufanya usafi ni la manispaa pekee.

Aidha, aliwataka kuacha kutupa taka ovyo na badala yake watupe sehemu maalum zilizotengwa ili kuondoa usumbufu kwa vijana wanaokusanya taka mitaani.

Pia, aliwataka wananchi walioamua kujitolea kushiriki katika zoezi hilo na kuomba kuendeleza zaidi sambamba na kuahidi kuwa Baraza la Manispaa litawaunga mkono kutokana na juhudi wanazozichukua.

Diwani wa Fuoni Mambosasa, Farashuu Mussa Abdalla na Sheha wa shehia hiyo, Asyah Omar Mohamed walisema hali ya usafi katika maeneo yao hayaridhishi.

Walisema wameamua kuanzisha zoezi la usafi kila mwezi ili kuifanya shehia yao iwe safi na ya kuvutia.

Walisema wameweka mikakati ya kutoa elimu na kukusanya taka katika shehia hiyo na kuahidi kuwachukulia hatua watakaochafua mazingira kwa makusudi.

Baadhi ya vijana wanaokusanya taka katika shehia hiyo walisema wanakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo kutolewa maneno yasiofaa, wananchi kukaidi kulipia ada ya uzoaji taka pamoja ukosefu wa vitendea kazi.

# Kasi ya UVCCM yaikosha CCM

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimeridhishwa na kazi zinazofanywa na Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM).

Alisema ni vyema kile kinachofanywa na umoja moja huo kiwe changamoto kwa jumuiya zingine za chama ili kuyafikia malengo.

Dk.Mwinyi alisema hayo wakati akizungumza na wajumbe wa Baraza Kuu la UVCCM Taifa, Ikulu Zanzibar alipowaalika kwa chakula cha jioni baada ya kufanikisha kampeni ya kijana kijani iliyofanyika mwishoni mwa wiki.

Pamoja na mambo mengine aliwahakikishia vijana kuwa serikali inajipanga kuendelea kujenga viwanja zaidi vya michezo ili kuinua vipaji.

Hivyo, aliwataka vijana kuhimiri propaganda za wapinzani na kuwahimiza kuhubiri amani, upendo na umoja wakati wote.

Naye Katibu Mkuu wa UVCCM Taifa, Jokate Mwegelo, alisema vijana wana wajibu wa kuacha alama katika chama kutokana na nyadhifa wanazopatiwa na taifa.

Mwenyekiti wa UVCCM Taifa, Mohamed Kawaida, alisema kuwa mwitikio wa kampeni ya kijana na kijani imetoa dira, mwelekeo wa namna gani UVCCM itaingia katika uchaguzi kuipatia CCM ushindi wa kishindo.

Katika hatua nyingine, Dk. Mwinyi, akifungua Kongamano la Vijana la Kitaifa visiwani hapa, lililobeba kauli mbiu ‘Kuwa kijana wa tofauti’, alisema serikali imejipanga kuhakikisha vijana wanapata elimu bora inayohitajika katika soko la ajira.

Aliwahakikishia vijana kuwa serikali itaendelea kuwekeza katika miundombinu ya elimu ya ufundi, ujuzi, na maarifa kwa ajili ya kuwajengea vijana uwezo.

Pia, aliwataka vijana kuchangamkia fursa zinazoandaliwa na serikali kwa lengo la kuzifikia ndoto zao.

# Ukosefu taarifa sahihi chanzo wafugaji kutoendelea

**Na Mwandishi Wetu**

UKOSEFU wa taarifa sahihi za ufugaji imetajwa ni mojawapo ya changamoto inayowakabili wafugaji wengi nchini.

Mkurugenzi wa kampuni inayojihusisha na utatuzi wa changamoto za wafugaji SAB, Saida Bwanakheri, alieleza hayo juzi wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya wafugaji kuku yaliyoandaliwa kwa ushirikiano na Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani.

Alisema wafugaji wanatakiwa kusaidiwa kwasababu ndiyo wateja wakubwa wa ununuzi wa chakula cha mifugo.

“Nimeona wafugaji ndiyo chachu ya maendeleo yetu, hivyo tujitoe kwao kwani soko letu linazidi kutanuka kwasababu yao. Hivyo badala ya kumuuzia mifuko miwili ya chakula ataweza kununua mifuko mingi zaidi,” alisema Saida.

Pia aliwataka wananchi wa wilaya hiyo kuendelea kujitokeza katika kupata elimu ya ufugaji kuku wa kisasa ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Alisema hali ya hewa ya Kisarawe inaruhusu ufugaji kwani maeneo yapo mengi, hivyo viongozi wapo tayari kuwashika mkono katika kupata fursa hio.

Alisema: “SAB tunawaahidi wananchi wa Kisarawe kupata tuzo ya ufugaji kuku kwani Kisarawe imekua ikuchukua tuzo ya ufugaji ng’ombe tu lakini msimu ujao tutakwenda kuendelea kuiheshimisha katika masuala ya ufugaji kuku.”



Mwanasheria wa Chama cha ACT-Wazalendo ambaye ni Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaman, akizungumza katika mkutano wa hadhara wa chama hicho uliofanyika Jimbo la Magomeni Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT Wazalendo: Tutaendelea kuonyesha upungufu

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kazi ya vyama vya upinzani ni kusimamia serikali iliyopo madarakani kwa kuonesha upungufu.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Ismail Jussa Ladhu, alisema hayo alipokuwa akihutubia mkutano uliofanyika Uwanja wa Ayoub Jimbo la Magomeni Mkoa wa Mjini Magharib Unguja.

Alisema kazi hiyo ndiyo inayofanywa na ACT Wazalendo ikiwamo kufichua vitendo vya ufisadi hasa katika miradi ya ujenzi.

“Kazi ya chama cha siasa cha upinzani cha kwanza ni kuisimamia serikali iliyopo madarakani kwa kuonesha uovu, ufisadi, kutowajibika ili wananchi waweze kupima na la pili ni kutangaza mbadala wa sera,” alisema Jussa.

Alisema mpaka sasa miradi 27 Zanzibar inakabiliwa na matatizo licha ya kuzungumza hadharani lakini hakuna hatua zozote za kisheria zilizochukuliwa.

“Sisi tunaushahidi wa kutosha kwa kila tunachokizungumza ikiwamo miradi 27 inayokabiliwa na tatizo la ufisadi na kama tunasema uongozi serikali iruhusu Tume Huru ya Kimataifa ije Zanzibar kufanya uchunguzi ili ukweli ujulikane,” alisema.

Aliitaja baadhi ya miradi ambayo inakasoro ni ujenzi wa hospitali 10 za wilaya na moja ya mkoa, ujenzi wa shule, mradi wa kununua nguzo za umeme, mradi wa ununuzi wa boti.

Mingine ni ukodishwaji wa visiwa vidogo, Uwanja wa Gombani, mfuko wa manunuzi, ukodishwaji wa mejengo wa Mji Mkongwe na huduma za Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume.

Mwenyekiti wa chama hicho, Othman Masoud Othman, alisisitiza umuhimu wa misingi ya utawala bora ikiwamo kiongozi kupatikana kwa njia za halali kupitia uchaguzi.

# Kauli mbili zuio mikutano ya hadhara zazua jambo

**Na Jenifer Gilla**

KAULI mbili za Jeshi la Polisi kuhusu mikutano ya hadhara zimezua mjadala:

Chama cha ACT-Wazalendo kimeandikiwa barua kuwa mikutano imezuiwa; na Msemaji wa Jeshi la Polisi ameeleza kuwa mikutano inayofuata sheria haijazuia.

Mwandishi wa Nipashe aliiona jana barua kwenye ukurasa wa X wa ACT-Wazalendo yenye kumbukumbu namba EA.612/795/01/17 iliyotiwa saini na Kaimu Mkuu wa Polisi Wilaya ya Mbagala, SP Robert John kwenda kwa ACT-Wazalendo Kata ya Charambe, Mbagala, mkoani Dar es Salaam.

Barua hiyo inaeleza kuwa Agosti 11 mwaka huu walipokea barua yenye kumbukumbu namba ACT/MBG/CHR/VOL.001/024, wakitoa taarifa ya kufanya mkutano wa hadhara.

"Pamoja na barua hii, ninapenda kukujulisha kuwa mikutano yote ya hadhara na ya ndani imezuiwa hadi hapo yatakapotolewa maelekezo mengine," Kaimu Mkuu wa Polisi Wilaya ya Mbagala, SP John anaeleza katika barua hiyo.

Vilevile, katika ukurasa wa X wa chama hicho, kinaelezwa kuwa viongozi wao watatu wamekamatwa na polisi wakati wakiendelea na mkutano wa kusherehekea Siku ya Vijana Duniani.

Kwa mujibu wa kilichoandikwa katika ukurasa wa X wa chama hicho, viongozi waliokamatwa ni Mwenyekiti wa Ngome ya Vijana Mkoa wa Dar es Salaam wa ACT- Wazalendo, Salumu Mkambula, Mwenyekiti wa Chama Kata ya Chalambe, Said Mlazi na Katibu wa Chama Kata ya Charambe, Mrisho Mliomi.

Licha ya viongozi hao kukamatwa, chama hicho kilisisitiza kuendelea na mhadhara wa Siku ya Vijana Duniani, ukiongozwa na Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu.

Jana mchana, Msemaji wa Jeshi la Polisi Makao Makuu ya Polisi Dodoma, Kamishna Msaidizi David Misime, alitoa taarifa kwa umma ikieleza kuwa mikutano haijapigwa marufuku.

"Jeshi la Polisi lingependa kutoa taarifa kuwa halijapiga marufuku kufanyika mikutano ya nje ya hadhara na ile ya ndani, mradi inafuata matakwa ya sheria.

"Kilichopigwa marufuku ni mkusanyiko uliokuwa umeitishwa na viongozi wa chama cha CHADEMA huko jijini Mbeya kwa kivuli cha kuadhimisha Siku ya Vijana Duniani," alisema.


## TANGAZO GARI LINAUZWA

Gari aina ya **TOYOTA HILUX** lenye namba za usajili **T164DXV** linauzwa lipo katika hali nzuri.

**Taarifa za Gari**

Aina ya gari: **Toyota Hilux**
Mwaka wa kutengenezwa gari: **2004**
Mafuta inayotumia: **Diesel**
Model Namba: **KF-LN167**
Uwezo wa injini: **2980**
Aina ya bodi: **Station Wagon**
Rangi ya gari: **Multi Colour**
Chesesi namba: **LN1670032032**
Namba ya injini: **5L5506667**
Kilometa ilizotembea: **110197**






KWA MAWASILIANO ZAIDI
Piga: 0757823350 / 0692793423





Makocha wa FC Barcelona wakiwa wamesimama na wachezaji chipukizi wa Chuo cha Soka cha Tanzanite kwenye kambi iliyofadhiliwa na Airtel Tanzania hivi karibuni huko Kunduchi, Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkandarasi ang'oa milango kisa deni

**Na Neema Sawaka, KAHAMA**

MKANDARASI wa kampuni ya AJ Mabao Investment, Abel Mabao, anadaiwa kung'oa milango ya Kituo cha Afya Bulige, katika Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga kwa madai ya kutokulipwa zaidi ya Sh. milioni 200.

Fedha hizo alizitumia kutekeleza miradi ya maendeleo na kupeleka vifaa vya ujenzi na kukamilisha ujenzi wa kituo hicho.

Tukio hilo limetokea mwishoni mwa wiki ambako kwa mujibu wa Mabao ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, aliingia mkataba wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD) na maabara kwa thamani ya Sh. milioni 44.5, lakini alilipwa Sh. milioni 35.5.

"Toka Agosti mwaka 2023, Mkurugenzi wa Halmashauri na jopo la wataalamu wake walinifuata ofisini na kuniomba kuwasaidia kusambaza vifaa vya ujenzi ili kukamilisha kituo hicho baada ya kuwa wamebanwa na Mkuu wa Mkoa wa kipindi hicho, Christina Mndeme,"

"Hata hivyo, mkuu huyo wa mkoa alipofika kituoni hapo kuweka jiwe la msingi alionesha kutokuridhishwa na kasi ya ujenzi na kubaini upungufu aliwataka wakamilishe ujenzi huo ili wananchi wapate huduma kwa wakati," alidai Mabao.

Alisema alitekeleza ujenzi Hospitali ya Wilaya ya Msalala na Chuo cha Afya Ntobo ambacho kinalipwa kwa malipo (CSR) na kuwa anaidai halmashauri hiyo zaidi ya Sh. milioni 200 na wamekuwa wakimpiga tarehe kila kukicha na kumpa ahadi hewa.

Alidai ahadi hizo zimekuwa hazitekelezeki hali ambayo iliwasukuma mafundi wanaomdai kwenda kwenye kituo cha afya kung'oa milango na kutaka kung'oa madirisha ya vioo vya aluminum ili wakauze kwingine waweze kulipa madeni yao.

Akizungumzia sakata hilo, kwa sharti la kutokutajwa jina, mmoja wa mafundi walioshiriki kung'oa milango hiyo, alidai kuwa tangu wamefanya kazi hiyo wamekuwa wakiishi kwa shida kutokana na kutokulipwa fedha zao huku na wao wakidaiwa na benki na watu binafsi.

"Muuguzi wa kituo hicho alipotuona tunang'oa milango aliwaita madereva bodaboda ili kutuzuia tusitoe milango, walifika hapo na kuhoji kinachoendelea ndipo waliambiwa mafundi wanaidai halmashauri hivyo walielewa na kuungana na wananchi waliokuwapo maeneo hayo kututazama," alisema fundi huyo.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Msalala, Hamis Katimba, alisema walipokea zaidi ya Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho kutoka Serikali Kuu na kituo hicho kilijengwa kwa ajili ya kuhudumia zaidi ya wakazi 18,184 wa kata hiyo na maeneo jirani.

Kuhusu madai hayo, Katimba alithibitisha kuwa mkandarasi huyo anaidai halmashauri yake kutokana na zabuni mbalimbali alizokuwa akitekeleza na kwamba kwa tukio hilo limefanywa na mafundi kung'oa milango kwa kuwa wanamdai mzabuni ambaye hajawalipa.

Alisema kufuatia tukio hilo ilimlazimu kuomba msaada kwa Mkuu wa Polisi Wilaya (OCD), asaidie kuwazuia mafundi hao wasiendelee kung'oa milango na kuondoka nayo.

"Ni kweli mzabuni anaidai halmashauri na kimsingi yeye alikuwa anavumilia na ametimiza mkataba wake na anachodai ni haki yake isipokuwa mafundi walikosa uvumilivu na siku mbili kabla ya kung'olewa milango hiyo nilikuwa nimeongea na mkandarasi wiki hii fedha zake atalipwa, lakini cha ajabu nikapokea taarifa hizo za mafundi kung'oa milango," alifafanua Katimba.


## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**BAHATI NYEURA MAREGERI** anatangaza kupotelewa na hati ya kusafiria yenye namba **TAE286557** iliyotolewa uhamiaji makao makuu mnamo tarehe 21/01/2020. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/164516/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MICHAEL REVOCATUS KIFYULA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. **S0114/0032** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SHULE YA SECONDARY KAENGESA SEMINARY** mwaka 2017, Cheti hiki kimepotea SUMBAWANGA. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/RUK/KAL/3898/2024**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**ELISON GODFREY MALISA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA PASSPORT NO, **TAE 574963** ILIYOTOLEWA NA OFISI YA UHAMIAJI 12 APRIL 2023 DAR ES SALAAM. YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA: **PHQ/ SHI/KAH/6831/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MAHOUA BAMBA PARUMS** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA RAV 4** yenye usajili namba **T 205 CD 720**, CHASSIS NAMBA: **ACA315040872** na ENGINE NAMBA: **2AZH277000.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/16492/2024**


**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE DISTRICT DELEGATED COURT OF MOROGORO AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.16831 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE LAURENT MATHEW JAKA-THE DECEASED**

**AND IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATION BY SUZANA MATHEW JAKA**
**SUZANA MATHEW JAKA..................................PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Made under rule 75 of the probate and administration of Estate rule, CAP 352 R,E 2019)**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above- named pepetitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 14th day of AUGUST,2024.

**DATED and SIGNED at Morogoro this 24th day of JULY 2024.**

Senior resident magistrate
Morogoro District Court

## HABARI KIMATAIFA

# Janga la kuporomoka jaa la taka, 23 wafariki dunia Uganda

**KAMPALA,** UGANDA

IDADI ya watu waliopoteza maisha katika janga la kuporomoka kwa jaa la taka mjini Kampala imefikia 23 huku makundi ya waokoaji wakizidi kupoteza matumaini ya kupata manusura.

Ilielezwa kuwa wengi wa waliofariki ni wakazi wa mtaa wa Lusanja ambao husaka riziki zao kutoka kwenye jalala la taka zinazoletwa kutoka sehemu mbalimbali za mji huo wenye idadi ya watu takribani milioni 4.

Ilibainishwa kuwa maporomoko hayo yalitokea juzi alifajiri, na kusababisha watu kunasa baada ya makazi yao kufunikwa na taka, wakiwa bado wamelala.

"Hadi sasa ni manusura 18 waliokimbizwa hospitalini. Lakini wakazi wanaelezea kuwa watu wengi bado wamenaswa na kadri muda unavyoyoyoma, hii ikiwa siku ya tatu ya shughuli za kujaribu kuwanusuru, matumaini ya kuwapata wakiwa wangali hai yanazidi kupukutika," walisema maofisa wa uokoaji.

Halmashauri ya Mji wa Kampala ilianzisha jaa hilo mwaka 1996. Na kwamba tangu wakati huo, wakaazi wa mtaa huo na maeneo jirani wamekuwa wakilalamikia kuhusu madhara yake kwa afya zao na mifugo yao kutokana na uvundo unaosababisha harufu mbaya katika eneo hilo. Aidha, ilielezwa kuwa kutokana na shughuli za watu waliochukua fursa za kusaka riziki kwa kuokota baadhi ya takataka kama plastiki na mabaki mengine na kuziuza kwa wanaozichakata ilisababisha kuvutia idadi kubwa ya wakaazi kujenga nyumba jirani na dampo hilo.

Msemaji wa wizara ya ofisi ya waziri mkuu inayoshughulikia majanga Charles Odongtho, alisema hatua wanazochukua kwa sasa ni pamoja na kuwapelekea misaada ya dharura wakazi hao.

"Watu 2000 wameathirika kutokana na janga hili na mbali na kuanzisha mpango wa kuwafidia tunashirikiana na Shirika la Msalaba Mwekundu kuwapa makao ya muda katika hema tulizokita eneo jirani," alisema Odongtho. Akitoa rambirambi zake kwa waliowapoteza jamaa zao, Rais Yoweri Museveni alikosoa mwenendo wa kuwaacha watu kuishi katika maeneo hatari kama hayo. Akiagiza uchunguzi wa mara moja kubaini waliohusika katika kutelekeza majukumu yao na kusababisha dampo hilo kuwa hatari.

Watu mbalimbali walionyesha kukubaliana na hatua ya kiongozi huyo, wakisema kuwa hiyo sio ajali ila ni uhalifu wa watendaji katika halmashauri ya mji kupuuzia usalama wa watu.

Mapema mwaka huu, meya wa mji wa Kampala alizuru eneo hilo na kukosoa mienendo ya ufisadi kuwa chanzo cha jaa hilo la taka kutoshughulikia ipasavyo ili hali kiasi kikubwa cha fedha hutolewa kuchakata taka hizo.

***DW***



Maofisa wa Msalamba Mwekundu wakishirikiana na wananchi waliojitokeza katika shughuli za uopoaji wa miili ya watu waliofunikwa na jaa la taka Kampala, jana. **PICHA: MTANDAO**

# Rais Kagame aanza rasmi muhula wa nne

**KIGALI,** RWANDA

RAIS wa Rwanda, Paul Kagame, ameanza rasmi kuhudumu kama rais kwa muhula wa nne baada ya kula kiapo, akisema amani ya kikanda ni kipaumbele chake katika kukabiliana na mzozo unaoendelea kwenye nchi jirani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Rais Kagame alikula kiapo juzi, baada ya kupata ushindi wa kishindo katika uchaguzi wa mwezi uliopita kwa kupata asilimia 99.18 ya kura, na kumpa fursa ya kukaa madarakani kwa miaka mingine mitano.

Zaidi ya marais 10 na viongozi wengine wa heshima kutoka mataifa ya Afrika walihudhuria hafla ya kuapishwa kwake mjini Kigali, ambako wengi walikuwa wamevalia bendera ya taifa yenye rangi ya kijani, njano na bluu.

Matokeo ya uchaguzi wa Julai 15 hayakushangaza kwa Kagame, ambaye ameliongoza taifa hilo dogo la Afrika ya kati tangu mauaji ya kimbari ya 1994.

"Amani katika kanda yetu ni kipaumbele kwa Rwanda, lakini haijapatikana, hasa mashariki mwa DRC," Kagame alisema katika hotuba yake ya kuapishwa.

"Lakini amani haiwezi kutolewa na mtu yeyote au kutoka popote hata kwa nguvu ya kiasi gani ikiwa pande husika haielewi kinachohitajika," alisema katika msemo ulioonekana kuilenga Kinshasa.

Ofisi ya Rais wa Angola, Joao Lourenco, ilisema kiongozi huyo ni miongoni mwa waliohudhuria hafla hiyo, na kwamba alitarajiwa kuwa na mazungumzo ya siri na Kagame kuhusu makubaliano ya kusitisha mapigano nchini DRC yaliyofikiwa mwezi uliopita kutokana na juhudi zake.

***VOA***

## Wafanyakazi Kenya kugomea uwekezaji wa India

**NAIROBI,** KENYA

MUUNGANO wa Wafanyakazi wa Sekta ya Usafiri wa Anga nchini Kenya umesema kwamba wafanyakazi wa Shirika la Ndege la Kenya na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege watagoma kuanzia Agosti 19, mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa jana, ikielezwa kuwa inatokana na pendekezo la uwekezaji kutoka kwa kampuni ya India, 'Adani Airport Holdings', katika uwanja mkuu wa ndege nchini humo.

Mgomo huo unaweza kusababisha usumbufu mkubwa kwa Shirika la Ndege la Kenya, Kenya Airways, na kwa shughuli za Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta mjini Nairobi.

Mkuu wa Muungano wa Wafanyakazi wa Usafiri wa Anga nchini Kenya, Moss Ndiema alisema "Tutafikiria upya nia yetu ya kushiriki katika hatua za kiviwanda... ikiwa tu mkataba wa 'Adani Airport Holdings Limited' utatelekezwa kwa ukamilifu."

Mwezi uliopita, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini Kenya ilisema pendekezo la uwekezaji kutoka kwa kampuni hiyo ni pamoja na njia ya pili ya ndege katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta.

Kampuni ya Adani Holdings kutoka India ya Adani Group, kupitia kampuni yake tanzu ya Adani Airport Holdings Limited, ilionesha nia ya kupanua Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta (JKIA).

Ilielezwa kuwa tayari, wawekezaji hao wametenga dola bilioni 1.85 zaidi ya Sh. trilioni 503 kupanua sehemu ya Uwanja wa Ndege wa Kimaitaifa wa Jomo Kenyatta.

Pia ilielezwa kuwa iwapo mchakato huo utaidhinishwa, basi kampuni hiyo kutoka India itakuwa imejihakikishia kukusanya asilimia 18 ya mapato yake ya kila mwaka, ndani ya miaka 30, tangu kuanza kwa uwekezaji huo.

Kampuni hiyo pia imelenga kubadilisha mwonekano wa JKIA, ikiwa ni pamoja na kujenga sehemu ya pili ya kurukia ndege ndani ya uwanja huo wa kimataifa nchini Kenya.

Mchanganuo zaidi unaonesha kuwa kampuni ya Adani itatumia dola milioni 750 zidi ya Sh. trilioni 2 kujenga jengo la abiria, sehemu ya maegesho ya ndege na ya kutokea. Mradi unaotegemewa kukamilika mwaka 2029.

***TRT***

# DODOMA JIJI HAWAJAMALIZA, WAENDELEA KUSHUSHA VIFAA

**Na Adam Fungamwango**

ZIKIWA zimesalia siku mbili kabla ya kufungwa kwa dirisha kubwa la usajili, Klabu ya Dodoma Jiji imeendelea kufanya usajili ili kukiimarisha kikosi chao kwa msimu ujao wa Ligi Kuu, ambapo imefanikiwa kupata saini ya mchezaji, Emotan Cletus Eba, kutoka Tabora United.

Taarifa iliyotokea na Idara ya Habari na Mawasiliano ya klabu hiyo, imesema kuwa imemsajili mchezaji huyo anayezimudu nafasi ya kiungo mkabaji na mashambuliaji ili kukipa nguvu kikosi chao kwani kinataka kwenda kupigana kusaka nafasi nne za juu msimu ujao.

„Tumempata Emotan, ni mchezaji mzuri sana ambaye anaichangamsha safu ya kiungo ya timu hii, kikubwa tunawaambia mashabiki wa Dodoma Jiji kuwa hatujamaliza kusajili," ilisema sehemu ya taarifa ya klabu hiyo.

Kabla ya kujiunga na Tabora United, mchezaji huyo raia wa Nigeria, alikuwa akichezea Klabu ya River United, na hivi sasa ameamua kuipa kisogo timu hiyo na kwenda Makao Makuu ya nchi.

Timu hiyo imefanya usajili mkubwa kuelekea Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao kwani tayari ilishanasa saini ya Waziri Junior kutoka KMC, Reliants Lusajo, aliyesajiliwa kutoka Mashujaa FC, Ibrahim Ajibu (Coastal Union), Heritier Lulihoshi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Daudi Milandu, Dickson Mhilu na Allain Ngeleka, kipa raia wa DR Congo, ambao wamejiunga na timu hiyo wakitokea, Kagera Sugar.

Timu hiyo itacheza mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu msimu huu, Jumamosi ijayo itakapokuwa ugenini, Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, kuivaa, Mashujaa FC.




Wananchi wa Mtaa wa Panga Tegeta Wazo, Dar es Salaam, wakitoa kilio chao kwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, cha kutaka kusitishwa ujenzi wa Shule ya Msingi katika eneo hilo ambalo lilitengwa kwa ajili ya shughuli za michezo tangu mwaka 1978. **MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaingilia kati ukiukwaji matumizi Uwanja wa Panga

**Na Shufaa Lyimo**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, ametoa siku tatu kwa Halmashauri ya Kinondoni kuhakikisha Uwanja wa Mpira wa Miguu wa Panga, uliopo Tegeta, Dar es Salaam unarudishwa kwenye matumizi yake kama ilivyokuwa hapo awali.

Agizo hilo alilitoa jana baada ya kuwasikiliza wananchi waliokuwa wakilalamikia hatua ya Mwenyekiti wa Mtaa wa Wazo kwa kushirikiana na Diwani wao, kuagiza pajengwe shule pasipo kushirikisha wakazi wa eneo hilo.

Uamuzi huo wa kujengwa shule ulizua mgogoro kati ya viongozi hao na wananchi, hivyo waziri huyo mwenye dhamana ya michezo nchini akachukua hatua ya kwenda kuwasikiliza kabla ya kutoa agizo hilo.

Dk. Ndumbaro alisema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, ametoa agizo maeneo yote yalitotengwa kwa ajili viwanja vya michezo yaliyopo wazi yasitumike kwa matumizi mengine.

„Natoa siku tatu kwa Halmashauri ya Kinondoni kuhakikisha uwanja huu unatumika kwa shughuli za michezo na si vinginevyo," alisema Ndumbaro.

Alisema maagizo hayo yametolewa na Rais Samia kuwa eneo hilo lisijengwe shule kama ilivyoripotiwa na badala yake viongozi hao wakae na wananchi watafute eneo lingine la ujenzi wa shule.

Vile vile alimtaka mkandarasi wa wa shule hiyo asitishe ujenzi huo haraka iwezekanavyo na kumwahidi kumpatia tenda nyingine haraka iwezekanavyo.

# Pamba Jiji FC yaionya Prisons

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Pamba Jiji imeahidi kufanya vema kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, ikianza katika mechi yake yake ya kwanza dhidi ya Prisons, Ijumaa ijayo.

Akizungumza jijini Mwanza, Mkuu wa Mkoa huo, Said Mtanda, amesema baada ya kuipandisha daraja timu hiyo, matarajio yake sasa ni kuiona inafanya vema katika mechi za Ligi Kuu, ikianza dhidi ya Prisons.

Alisema ni matarajio yake kuona timu inafanya vizuri, akiwataka mashabiki wa timu hiyo kuiunga mkono kwa kujitokeza kwa wingi katika mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu.

Pamba Jiji imepangwa kufungua msimu wa Ligi Kuu 2024/25 kwa kucheza dhidi ya Prisons Ijumaa ijayo ikiwa nyumbani, CCM Kirumba.

"Ni matarajio yangu Pamba itafanya vizuri katika Ligi Kuu tukianzia Ijumaa na sisi tukiwa wenyeji Uwanja wa CCM Kirumba, tukicheza na timu ya Prisons.

Kwa hiyo ninaomba wana Mwanza wote, tuendelee kuiunga mkono timu ya Pamba Jiji kwa sababu ndiyo kitu chetu cha kujivunia," alisema Mtanda.

Itakuwa ni mechi ya kwanza kwa timu hiyo kucheza Ligi Kuu tangu iliposhuka daraja mwaka 2001, na kufanikiwa kupanda msimu huu, ikishika nafasi ya pili katika Ligi ya Championship.

Katika kujipima nguvu, Pamba ilicheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Vital'O ya Burundi Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa CCM Kirumba na kulazimishwa sare ya bao 1-1.

Ilikuwa ni mechi ya Tamasha la Pamba Day, ambapo pamoja na mambo mengine, ilitambulisha wachezaji na benchi lake la ufundi, pamoja na burudani kadhaa kabla ya mechi hiyo, ambayo mabao yake yaliyofungwa na Erick Okutu dakika ya 55 kwa upande wa Pamba na wageni kusawazisha kupitia kwa Hakizimana Ramadhani dakika ya 79.



## ZISIKUPITE

### BERGE ATAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inaweza kumjaribu kiungo wa kati wa Burnley na Norway, Sander Berge mwenye umri wa miaka 26, kwenda Old Trafford kwa kumpa mkataba wa kulipwa mshahara wa pauni 100,000 kwa wiki. ***(Sun)***

### TRIPPIER NA WEST HAM

WEST Ham inavutiwa na beki wa kulia wa England, Kieran Trippier, huku mustakabali wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, huko Newcastle United ukiwa bado haujaamuliwa. ***(Telegraph)***

### ZUBIMENDI KUTUA LIVER

KIUNGO wa kati wa Hispania, Martin Zubimendi, anatarajiwa na Real Sociedad kukubali kuhamia Liverpool, ingawa klabu hizo bado zinahitaji kuafikiana dili la mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Athletic)***

### BROJA KUAMUA HATIMA

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Albania, Armando Broja, atafanya mazungumzo na kocha Enzo Maresca, kufahamu mustakabali wake. Everton na Wolves ni miongoni mwa klabu zinazomtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(Mail)***

### CHALOBAH AVUTIA

WEST Ham inavutiwa na mlinzi wa Chelsea, Trevoh Chalobah mwenye umri wa miaka 26, na beki wa kati wa Ujerumani, Mats Hummels (35), ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Borussia Dortmund. ***(Sky Sports)***

### PALACE PIA INAMTAKA

KLABU ya Crystal Palace pia inamtazama mlinzi wa Chelsea, Trevoh Chalobah, na beki wa Wolfsburg ya Ufaransa, Maxence Lacroix mwenye umri wa miaka 24, kama chaguo lao la beki wa kati. ***(Telegraph)***

### CASTLEDINE AWINDWA CHELSEA

CHELSEA imewasiliana na Rangers kuhusu uwezekano wa kumnunua kiungo wa kati wa akademi mwenye umri wa miaka 19, Leo Castledine. Aberdeen pia inavutiwa na Mwingereza huyo. ***(FootballScotland)***

### BEIER AVUTIA

LIVERPOOL bado inavutiwa na mshambuliaji wa Ujerumani na Hoffenheim, Maximilian Beier, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, anataka kujiunga na Borussia Dortmund na yuko kwenye mazungumzo na klabu hiyo ya Bundesliga. ***(Sky Germany)***

### BELLA-KOTCHAP AKATALIWA

KLABU ya Southampton imepokea ofa kutoka Hoffenheim kwa mlinzi wa miaka 22, Armel Bella-Kotchap. ‚The Saints' hao tayari wamekataa ofa ya pauni milioni 8.6 kutoka Stuttgart. ***(Sky Germany)***

### DIGNE HAITAKI GALATASARAY

MLINZI wa Aston Villa, Lucas Digne, amekataa pendekezo la kujiunga na Galatasaray. Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 31, anatarajiwa kubaki na Villa. ***(Athletic}***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# VAN DIJK: BADO SIJAPATA OFA YA MKATABA MPYA

**Hakuna mabadiliko kwa sasa, jambo la msingi ni kuwa na imani na tutaona kitakacho...**

**LIVERPOOL, England**

VIRGIL van Dijk amesema Liverpool bado hawajampa mkataba mpya, licha ya mkataba wake wa sasa kuelekea kumalizika mwishoni mwa msimu huu mpya wa 2024-25.

Van Dijk, nahodha wa klabu, ni mmoja wa wachezaji watatu muhimu ambao wako katika mwaka wa mwisho wa mkataba wake pamoja na Mohamed Salah na Trent Alexander-Arnold.

„Hakuna mabadiliko kwa sasa," alisema Van Dijk baada ya Liverpool kushinda mabao 4-1 kabla ya msimu mpya dhidi ya Sevilla Uwanja wa Anfield juzi, Jumapili.

Liverpool bado hawajafanya usajili wowote wakati wa dirisha la usajili la majira ya kiangazi, tangu kuwasili kwa Arne Slot kuchukua nafasi ya Jurgen Klopp, lakini Van Dijk anatumai kuwa nyongeza itawasili.

„Ni wazi nadhani tunapaswa kufanya usajili kulingana na msimu utakwenda kwa muda gani, lakini nadhani wanafanya kazi nyuma ya pazia na nina imani na klabu kwamba watafanya jambo sahihi kwa ajili yetu na kupata kikosi bora zaidi, ili tuweze kushindana katika kila shindano tulilonalo," alisema.

„Hilo ndilo jambo la msingi ninalozingatia, kuwa na imani na tutaona kitakachotokea. Nadhani wanafanya kazi kwa bidii nyuma ya pazia, tutaona jinsi hiyo itaisha."

# NETO RASMI SASA MALI YA CHELSEA




**LONDON,** England

CHELSEA imekamilisha usajili wa Pedro Neto kutoka Wolverhampton Wanderers, klabu hiyo ya London Magharibi juzi, Jumapili.

Winga huyo wa Ureno alisaini mkataba wa miaka saba na klabu yake hiyo mpya na kutambulishwa kwa mashabiki Stamford Bridge wakati wa mapumziko Chelsea ilipotoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Inter Milan katika mechi ya kirafiki ya kujiandaa na msimu mpya.

"Ninahisi kushukuru sana kujiunga na klabu hii," alisema Neto katika taarifa yake.

"Nimefanya kazi kwa bidii sana katika taaluma yangu kuwa hapa na ninatazamia kuingia uwanjani na jezi hii."

Neto mwenye umri wa miaka 24, ameifanya Chelsea ifikishe pauni milioni 200 baada ya kulipa pauni milioni 51.3.

Tayari klabu hiyo imewasajili Omari Kellyman kutoka Aston Villa, Tosin Adarabioyo wa Fulham, Marc Guiu (Barca), Kiernan Dewsbury-Hall (Leicester City), Renato Veiga (Basel), Caleb Wiley (Atlanta United), Filip Jorgensen (Villarreal) na Aaron Anselmino kutoka Boca Juniors.

Chelsea wataanza kampeni zao za Ligi Kuu England 2024-25 chini ya kocha mpya, Enzo Maresca dhidi ya Manchester City Jumapili wiki hii.

# Ederson afichua mustakabali wake City

**MANCHESTER,** England

EDERSON amebainisha mustakabali wake Manchester City, na kunyamazisha uvumi unaomhusisha mlinda mlango huyo kuondoka msimu huu wa majira ya joto.

Mbrazil huyo amekuwa akikabiliwa na tetesi nyingi za uhamisho msimu huu wa majira ya joto, huku kukiwa na uwezekano mkubwa wa kuhamia Saudi Arabia.

Hata hivyo, mlinda mlango huyo amechagua kuendeleza soka lake akiwa na mabingwa hao wa Ligi Kuu England.

Ederson alizungumzia mustakabali wake baada ya ushindi wa Ngao ya Jamii wa City dhidi ya Manchester United, akifichua mazungumzo aliyokuwa nayo na kocha Pep Guardiola.

"Imekwisha. Nilizungumza na baadhi ya wachezaji, kocha, mkurugenzi na kila mtu," alisema akiiambia ESPN Brasil.

"Nilizungumza na familia yangu na ulikuwa uamuzi wa pamoja. Tutakaa miaka mingi zaidi City.

"Tayari nimeamua mustakabali wangu, haswa baada ya mazungumzo niliyofanya na Guardiola. Msimu huu, ninalenga kabisa City na wachezaji wenzangu kusaka mataji zaidi."

Ederson alishiriki katika mchezo wa Jumamosi wa Manchester dabi katika Uwanja wa Wembley, ambapo hata alipiga hatua katika mikwaju ya penalti.

Guardiola pia alichukua muda kuzungumza juu ya mustakabali wa Ederson ndani ya City, akithibitisha kwamba alikuwa na furaha kuona kipa huyo akibaki.

Bosi huyo kutoka Katalunya, anajivunia chaguo katika nafasi ya kipa - huku Stefan Ortega akiwa chaguo la kutegemewa iwapo Ederson atakosekana.

Mjerumani huyo alicheza mechi 20 msimu wa 2023/24, ikiwamo mchezo wa fainali wa Kombe la FA dhidi ya Mashetani Wekundu huku Ederson akiuguza jeraha.

# Chelsea yamtaka Felix

**LONDON,** England

MPANGO wa Chelsea kumnunua mshambuliaji wa Atletico Madrid, Samu Omorodion umeshindikana, kwa mujibu wa ripoti nyingi, na badala yake klabu hizo mbili sasa ziko kwenye mazungumzo juu ya uhamisho wa Joao Felix.

'The Blues' walikuwa wamemtambua Samu mwenye umri wa miaka 20, kama mmoja wa washambuliaji wao wakuu mapema mwaka huu.

Mwanzoni, Atletico walikataa kufanya biashara, lakini walipunguza msimamo huo walipojaribu kufikia makubaliano na Conor Gallagher, huku pia wakitaka kumleta fowadi wa Manchester City, Julian Alvarez.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, dili zote tatu zilionekana kukamilika, lakini sasa ziko hatarini baada ya mpango wa Samu kwenda Stamford Bridge kushindikana.

Hapo awali Samu alikuwa amekubali mkataba wa miaka saba Chelsea, lakini ripoti kadhaa kutoka Ulaya zinadai kwamba kulikuwa na shida katika kusaini mkataba huu na uhamisho huu umezimwa.

Atletico wanahitaji kufanya mauzo makubwa ili kupata fedha zinazohitajika kwa Gallagher na Alvarez, ambao watagharimu pauni milioni 100.

Gallagher tayari yuko Madrid akisubiri uhamisho wake ufanyike, huku Alvarez akiwasili jijini humo jana Jumatatu kufanyiwa uchunguzi wa afya.

Fabrizio Romano alikuwa wa kwanza kuripoti Jumapili usiku kwamba Chelsea na Atletico sasa wako kwenye majadiliano juu ya Felix, ambaye alitumia kipindi cha pili cha msimu wa 2022/23 kwa mkopo Stamford Bridge.




Wakala wa Felix, Jorge Mendes, tayari yuko London akiwa ameisaidia 'The Blues' kumleta winga wa Wolves, Pedro Neto.

Fowadi wa Ureno, Felix alirejea Atletico kwa mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya baada ya kushindwa kupata uhamisho wa kuondoka.

Alijiunga na Barcelona kwa mkopo kwa msimu wa 2023/24, lakini 'La Blaugrana' haiko katika hali nzuri ya kifedha ya kumsajili jumla, wakati Aston Villa wameonesha nia wiki za hivi karibuni.

HABARI MICHEZO

# MSIGWA AVUTIWA UBORA WA BOKA MECHI YANGA, AZAM

**Na Shufaa Lyimo**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, amekunwa na kiwango kilichooneshwa na beki wa kushoto wa Yanga, Chadrack Boka, katika mchezo wa fainali wa Ngao ya Jamii 2024 dhidi ya Azam FC uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi.

Msigwa hakusita kueleza kuvutiwa kwake na beki huyo, wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika kwa mchezo huo ambao Yanga ilifanikiwa kubeba ngao hiyo kwa kuibuka na ushindi wa mabao 4-1.

"Boka ni mchezaji mwenye uwezo mkubwa, hawa ndio aina ya wachezaji ambao tunawahitaji kwa ajili ya kuliboresha soka la Tanzania," alisema Msigwa akiachilia furaha yake.

Aidha, aliwataka wachezaji wa Tanzania kuiga aina ya uchezaji wake ili waweze kupata nafasi ya kwenda kucheza soka la kulipwa nje ya nchi.

"Natamani wachezaji wetu waige aina ya uchezaji wake, ananifurahisha kwa kuwa anafahamu kile ambacho anakifanya ndani ya uwanja," alisema.

Katika hatua nyingine aliipongeza timu ya Yanga kutokana na kuendeleza ushindani wake na kuweza kutwaa ubingwa wa Ngao ya Jamii 2024 kwa kuifunga Azam FC mabao 4-1.

Boka ambaye amesajiliwa Yanga msimu huu, alianza kucheza soka katika klabu za nyumbani kabla ya kujiunga na FC Saint Eloi Lupopo ya Ligi Kuu ya DR Congo, na kuonesha uwezo mkubwa uliomfungulia milango ya kuitwa timu ya taifa.

Kwa upande wa timu ya taifa, Boka aliitwa kwa mara ya kwanza kuchezea DR Congo Agosti 28, 2022 na hadi sasa, ameicheza mechi sita.

Ametua Yanga kuchukua nafasi ya Mkongomani mwenzake, Joyce Lomalisa ambaye aliachana na Yanga baada ya mkataba wake kumalizika mwishoni mwa msimu uliomalizika.

## MWAMBAO MARATHON...



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Dk. Batilda Buriani (Kushoto), akipokea andiko la Chama cha Waandishi wa Habari za Michezo Tanzania (TASWA), kutoka kwa Mratibu wa Mbio za Taswa Mwambao Marathon, Mashaka Mhando. Andiko hilo ni kwa ajili ya kuomba udhamini wa mbio hizo zitakazofanyika jijini Tanga, Septemba 29, mwaka huu, hafla hiyo fupi ilifanyika katika ofisi za mkuu wa mkoa juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mashujaa yafunga usajili na Kibaya

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mashujaa FC, imefunga usajili wake kuelekea msimu ujao wa mashindano kwa kuinasa saini ya kiungo mshambuliaji na winga, Jaffar Kibaya, akitokea Singida Black Stars.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo jana, inasema kuwa Kibaya amesajiliwa baada ya benchi la ufundi la timu hiyo kuvutiwa na huduma yake, hivyo atakuwa mmoja wa wachezaji watakaoitumikia klabu hiyo kwa msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Taarifa hiyo ilieleza mchezaji huyo anafunga usajili wa msimu huu, ambapo sasa inabaki kazi ya Kocha Mkuu, Mohamed Abdallah ,Bares', kukiunganisha kikosi hicho ili kuleta matokeo chanya.

Kabla ya kujiunga na Singida Black Stars, Kibaya, alikuwa mmoja wa wachezaji tegemeo katika kikosi cha Mtibwa Sugar kwa misimu kadhaa wakati kiko Ligi Kuu.

Mashujaa FC, ambayo itakuwa ni msimu wake wa pili wa Ligi Kuu, itaanza kumtumia mchezaji huyo Jumamosi ijayo, ikiwa nyumbani, Lake Tanganyika, kucheza dhidi ya Dodoma Jiji.

Kabla ya kumnasa Kibaya, ilifanya usajili wa Seif Karihe kutoka Mtibwa Sugar, Chrispin Ngushi wa Yanga, Abdulmalik Zacharia akitokea Namungo, straika wa zamani wa Simba, Mohamed Mussa, Carlos Protus, Mathew Michael, Ismail Mgunda, Robert Mathias, Ally Nassor ,Ufudu' na wengineo.

Jumamosi iliyopita ilitesti mitambo yake ikicheza dhidi ya Inter Star ya Burundi kwenye mechi ya Kilele cha Tamasha la Mashujaa Day na kuichakaza mabao 4-1, yakiwekwa wavuni na Abdulnasir Gamal, Ismail Mgunda, Nyenyezi Juma na Mundhir Vual.

## Simba sasa yaleta straika Mcameroon

INATOKA UK. 24

"Mpaka sasa Simba imeonekana kuwa na wachezaji wenye viwango vikubwa mno, kilichobaki ni mwalimu kutengeneza timu yenye mtiririko, muunganiko na maelewano ya pamoja.

"Eneo pekee linalohitaji nguvu mpya ya nje ni eneo la ushambuliaji, nalo viongozi wetu wanakamilisha mpango hivi punde, Wanasimba tuwe na subira tumpe nafasi kocha kufanya kazi yake, tutakapoanza kula matunda ya furaha kila mtu apate tunda lake," alisema Ahmed.

## Gamondi: Tupo tayari mechi CAF

INATOKA UK. 24

timu nyingine isiyokuwa na aina ya wachezaji wakomavu wangetoka mchezoni baada ya kufungwa bao la kwanza, lakini wachezaji wangu walitulia, wakashauriana nini la kufanya, mpira wa miguu hauhitaji hisia kwa wachezaji, kinachotakiwa kutumika ni weledi tu, na nilisema huko nyuma na ninarudia tena, tunacheza kama tupo mazoezini, na hata leo hii (juzi) tumewaonesha watu kuwa huwa tunacheza kama tupo kwenye mazoezi.

"Mechi hizi mbili zimenipa mazoezi ya kutosha ya nini cha kwenda kufanya katika Ligi ya Mabingwa Afrika, naona tumekuwa tayari kwa michuano," alitamba kocha huyo ambaye kikosi chake Jumamosi kitakuwa uwanjani dhidi ya Vital'O, katika mechi ya hatua za awali Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwa upande wa Kocha wa Azam FC, Youssouph Dabo, alisema walishindwa kuudhibiti mchezo baada ya kutangulia kupata bao na kwamba ukosefu wa uzoefu kwa wachezaji wake ndicho kilichomwangusha zaidi.

Alisema baada ya kupata bao wachezaji wake hawakuwa na uwezo wa kuudhibiti mchezo, badala yake kuwapa nafasi wapinzani wao kufanya wanavyotaka uwanjani.

„Tulianza vizuri, tuliwazuia na kuwabana vilivyo mpaka tukafunga bao, lakini baada ya hapo wachezaji wangu hawakuonesha kama wana uzoefu wa nini cha kufanya baada ya kupata bao.

Wachezaji wetu hawakuonesha kuwa, wana uzoefu wa kuudhibiti mchezo baada ya kuwa wanaongoza, hivyo inabidi tujifunze, angalia hii si Ligi Kuu wala Ligi ya Mabingwa, lakini imekuwa hivi," alisema Dabo kwa masikitiko.

Yanga imetwaa taji la Ngao ya Jamii baada ya kulikosa msimu uliopita ilipofungwa na Simba kwa mikwaju ya penalti 3-1, Uwanja wa Mkwakwani, Tanga, Agosti 13 mwaka jana.

Ushindi huo umeifanya kutwaa taji hilo mara nane, ikicheza mara 15, ikilikosa mara saba, ikiwa kwenye nafasi ya pili chini ya Simba inayoongoza kuchukua Ngao ya Jamii mara nyingi zaidi, ikifanya hivyo mara 10, ikicheza mara 15, na kupoteza fainali tano.

Michezo
Jumanne Agosti 13, 2024
Nipashe

## Van Dijk: Bado sijapata ofa ya mkataba mpya

UKURASA 21






Wachezaji wa Yanga wakisherehekea baada ya kukabidhiwa Ngao ya Jamii kwa kuifunga Azam FC 4-1 katika mechi ya fainali iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Simba sasa yaleta straika Mcameroon

## Alikuwapo kikosi cha Cameroon cha AFCON, avutiwa na mradi wa Msimbazi, kila kitu...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha Mkuu, Fadlu Davids, akisema kama wachezaji wake wangekuwa makini juzi basi wangeimaliza mechi dhidi ya Coastal kipindi cha kwanza, Klabu ya Simba iko kwenye hatua za mwisho kumsajili straika Christian Leonel Ateba, kutoka Klabu ya USM Alger ya Algeria.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo na vyanzo vingine barani Afrika zinasema mchezaji huyo raia wa Cameroon, mwenye umri wa miaka 25, amekubali ofa ya Simba na kila kitu kimekwenda vizuri, kilichobaki ni klabu hiyo kumalizana na Waalgeria hao.

"Tunakamilisha dili la kumchukua straika Mcameroon, Ateba, tayari yeye mwenyewe amekubali kujiunga na Simba, na sasa tupo kwenye mazungumzo na klabu yake kuhusu ada ya uhamisho, tukimalizana tu atatua kabla ya kufungwa kwa dirisha kubwa la usajili, keshokutwa, Agosti 15," alisema mtoa taarifa ndani ya klabu hiyo.

Kabla ya kujiunga na USM Alger, mchezaji huyo alizichezea Klabu ya FC Yaounde 2017, kabla ya kujiunga na AS Etoa Meki, 2018 mpaka 2019, ambapo alitimkia AS Fortuna de Mfou, mpaka 2021, alipokwenda kujiunga na klabu ya Cotonsport Garoua ambapo alichezea hadi 2022, alipokwenda PWD Bameda, timu zote hizo zikiwa za nchini Cameroon, kisha akatoka nje ya mipaka ya taifa lake na kwenda Algeria kujiunga na USM Alger mwaka 2023.

Straika huyo pia alikuwa mmoja wa wachezaji 27 waliounda kikosi kilichocheza fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023, nchini Ivory Coast.

„Kama tutafanikiwa basi kuna mchezaji mmoja wa kigeni tutaachana naye au tutamtoa kwa mkopo kabla ya dirisha kufungwa," alisema mtoa taarifa wetu kwa sharti la kutotajwa jina.

Habari zinasema, wachezaji ambao wapo hatarini kuondoka kwenye klabu hiyo kumpisha straika huyo ni Ayoub Lakred, Freddy Michael au Fabrice Ngoma.

Baada ya kumalizika kwa mechi ya kusaka mshindi wa tatu wa Ngao ya Jamii, bado kocha Fadlu alikuwa akilalamikia safu yake ya ushambuliaji kutofanya vema licha ya kutengeneza nafasi nyingi.

Alisema katika mchezo dhidi ya Coastal Union, ilipaswa washinde mabao hata 5-0 hadi mapumziko, au angalu matatu tu na wangekuwa wameimaliza mechi mapema kiasi cha kwamba mchezo usingekuwa mgumu kipindi cha pili.

"Tulianza mchezo vizuri, tulifanya kila kitu ikiwa ni pamoja na kutengeneza nafasi, lakini tulishindwa kuiua mechi kipindi cha kwanza, tungeweza kupata mabao matatu, manne au hata matano. Kipindi cha pili hakikuwa kizuri sana, mwishoni tukacheza pungufu, inawezekana wachezaji wangu walikuwa wamechoka kutokana na mechi iliyopita, pili kucheza mechi mfululizo, ila mimi siiangalii timu hii kwa mechi moja au mbili, naiangalia kwa msimu mzima," alisema.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, aliwahakikishia wanachama na mashabiki wa Simba kuwa wanalifanyia kazi eneo la ushambuliaji.

INAENDELEA UK. 23

## Gamondi: Tupo tayari mechi CAF

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema ushindi wa mabao 4-1, walioupata juzi kwa kiasi kikubwa umetokana na uzoefu na ukomavu wa wachezaji wake na kwamba sasa tayari wameiva kwa ajili ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Gamondi, amesema wachezaji wake hawakuhamaki wala kuvunjika nguvu walipofungwa bao la mapema, badala yake walitulia na kufanya kile ambacho kinatakiwa kufanywa na wachezaji wenye ukomavu na uzoefu.

"Ninajivunia mimi binafsi na timu yangu ya Yanga kutwaa taji hili, tumecheza mpira mzuri, tulianza kwa kuruhusu bao, lakini hatukutetereka, baadaye tumekuja kupata matatu, kipindi cha pili tukafanya kazi ya kumiliki mpira, mwishoni tukapata la nne, uzoefu, ukomavu umetufanya kushinda mechi hii," alisema raia huyo wa Argentina.

Katika mechi ya fainali ya Ngao ya Jamii iliyochezwa juzi, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Yanga iliruhusu bao dakika ya 13, likifungwa na Feisal Salum, lakini ikasawazisha dakika tano baadaye likifungwa na Prince Dube, Yoro Diaby akijifunga dakika ya 28, Stephane Aziz Ki, akipachika la tatu dakika ya 31, kabla ya Clement Mzize kupigilia msumari wa mwisho dakika za majeruhi.

"Na kuthibitisha hilo, ingekuwa

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002